

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Sitini na Moja – Tarehe 29 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza Kikao chetu cha Sitini na Moja, Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):

Taarifa ya Mwaka ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*Workers Compensation Fund*) kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2016.

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2016.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali la Mheshimiwa Mulugo, Mbunge wa Songwe.

Na. 510

Hospitali ya Kanisa Katoliki – Mbeya (Songwe)

MHE. PHILIP A. MULUGO aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuipandisha hadhi Hospitali Teule ambayo inamillikiwa na Kanisa Katoliki Dayosisi ya Mbeya iwe Hospitali Teule ya Wilaya ili wananchi wa Songwe waweze kupata huduma stahili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 2 Januari, 2018, Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ilisaini mkataba na Kanisa Katoliki, Jimbo la Mbeya uliopandisha hadhi ya Hospitali ya Mwambani kuwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Songwe. Kufuatia mkataba huo, Serikali imeongezea fedha za ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa hospitali hiyo kutoka shilingi milioni 27.5 kwa mwaka 2017/2018 hadi shilingi milioni 105 kwa mwaka 2018/2019. Mkataba huo utaendelea hadi Serikali itakapokamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya

Songwe, ambayo katika mwaka wa fedha 2018/2019 imetengewa shilingi milioni 1.5.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mulugo, swali la nyongeza.

MHE. PHILIP A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, amenitendea haki. Kwa kweli katika mwaka huu, leo nina furaha kubwa sana, kwanza Serikali imenipatia shilingi milioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Songwe, nimefarijika sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mwanzo wa mwezi huu alikuja Dkt. Kalindu kutoka Hospitali ya Mwambani kuleta tatizo hili kwa ajili ya kuteuliwa Hospitali Teule ya Wilaya. Kwa hiyo, Serikali leo imejibu kwamba imepandisha hadhi na mkataba wetu umekubaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa vile sasa imekubaliwa kuwa hospitali ya wilaya, naomba kujua ni lini kibali kitatoka, maana ndiyo imekuwa hospitali ya wilaya lakini watumishi pale ni wachache na tangu mwaka 2014/2015 hatujawahi kupata vibali vya watumishi. Naomba nijue ni lini Serikali itatoa kibali cha kuajiri watumishi (madaktari na wauguzi) katika Hospitali ya Mwambani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mwalimu Mulugo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu, naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Mulugo kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia suala hili. Alikuja Daktari kutoka Hospitali ya Mwambani lakini pia na juzi imekuja Kamati ya Siasa ya Wilaya yake nao wakawa wanaulizia suala

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

hili. Kama ambavyo nilimuahidi tutafanya mapema na hili limewezeekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake anataka uhakika juu ya suala zima la kupata watumishi. Naomba nimhakikishie *process* ya ajira iko kwenye hatua za mwisho kabisa, zaidi ya wiki mbili tayari tutakuwa tushakamilisha suala la ajira na hakika tutahakikisha tunapeleka watumishi ili wakafanye kazi kwenye ile hospitali ambayo tumekubali itumike kama Hospitali ya Wilaya kwa sasa.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swalii lake.

Na. 511

Fidia kwa Wananchi wa Mekomario na Remong'oroni

MHE. BONIPHANCE M. GETERE aliuliza:-

Mnamo tarehe 12 Januari, 2018 Jeshi la Polisi lilifanya msako mkali katika Kijiji cha Mekomario – Bunda na katika msako huo wananchi wa eneo hilo waliharibiwa mali zao kama ilivyothibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Bunda na kutangazwa kwenye vyombo vya habari yaani *Star TV* tarehe 15 Februari, 2018:-

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya kulipa fidia wananchi kutokana na uharibifu huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambaye anaongoza Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na

Usalama za Mkoa na Wilaya, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 12 Januari, 2018 zilienezwa tetesi katika Kijiji cha Mekomariro, Wilayani Bunda kwamba wezi kutoka katika Kijiji cha Remong'oroni, Wilayani Serengeti walikuwa wameiba mifugo ya wakazi wa Mekomariro. Badala ya kutoa taarifa Polisi ili wasaidiwe kitaalam kupitia uchunguzi wa Polisi kubaini walioibowi na idadi ya mifugo iliyoiobiwa, walijikusanya kwa utaratibu usiokubalika na kwenda katika Kijiji cha Remong'oroni, wakafanya vurugu zilizosababisha watu wawili wakazi wa Kijiji cha Remong'oroni kuuwawa kikatili na wakamteka mtoto mmoja wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za ghasia hizo ziliporipotiwa Polisi, msako ulifanyika kuwabaini wahusika ambapo watuhumiwa nane wamefunguliwa mashtaka Mahakamani kwa kesi ya mauaji Na. RM 02/2018 ambayo bado inaendelea. Msako uliofanyika pamoja na ule wa watuhumiwa wengine waliojificha unaoendelea haujasababisha uharibifu wa mali za wananchi wa Mekomariro wala wa Remong'oroni. Kwa kuwa kesi inaendelea, nashauri tusubiri uamuzi wa Mahakama ili tupate ufumbuzi wa kisheria wa suala hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Getere, swalii la nyongeza.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati fulani hili Bunge haya majibu tunayopewa tuwe tunayachunguza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 ambayo wameisema hapa, ni kweli kulitokea vurugu na mimi kama kiongozi, Mbunge nilipiga simu saa 12.00 asubuhi kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuwataarifu kwamba kuna vijiji viwili vinagombania ardhi na kuna watu wameenda kulima, akina mama wawili wakanyang'anywa ng'ombe

kwa upande wa pili, tulivyokuwa tumepewa taarifa hizo. Saa 12.00 asubuhi viongozi wote wa Mkoa na Wilaya wakasema wamepokea taarifa, Jeshi la Polisi limekwenda pale saa 11.00 jioni watu wamepigana mpaka wameuana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi msako uliofanyika saa 11.00 jioni, tarehe 13 tulienda pale viongozi wote, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa na vyombo vyahabari vilikuwepo, maduka yote yamechukuliwa. Mambo mengine kusema hapa ni aibu, nachokionomba Serikali katika hili ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza maswali.

MHE. BONIPHANCE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Serikali katika hili waende wakaangalie hiyo halisi ilivyokuwa na sisi tuna ushahidi wa kutosha juu ya jambo hilo. Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa chanzo cha mgogoro huo ni mgogoro wa ardhi ambao una vijiji vitatu ambapo kimsingi mgogoro ule ni kama umeisha. Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliyelewepo Mheshimiwa Simbachawene alishafika pale akatoa maamuzi, maeneo yale yamegawanywa na vizingi vimewekwa. Ni lini sasa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaenda kuweka *GN* kwenye maeneo hayo ili kumaliza mgogoro huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri la kwanza ni ushauri na ombi, la pili ndiyo swali, naomba ujibu hilo swali la pili.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uniruhusu nimsifu sana Mheshimiwa Boniphance Mwita Getere. Eneo

analoliongoza lina changamoto nyingi sana hususani hizi za kiulinzi na kiusalama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mweyekiti, ombi lake aliloliomba, kwa sababu uchunguzi wa kipolisi bado unaendelea, haujakamilishwa kabisa, napenda nimhakikishie kwamba uchunguzi ule utaendelea kufanyika kwa kufuata taratibu za sheria za Polisi na sisi kupitia Kamati zetu za Ulinzi na Usalama, Mkoa na Wilaya tutafanya tathmini ya kina kuangalia matatizo gani yalijitokeza ili tuweze kuyatatua tukishirikiana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, uwekaji wa *GN*kuondoa migogoro iliyokuwepo kwenye vijiji husika, naomba sana Mheshimiwa Mbunge awe na subira, suala hili linafanyiwa kazi kwa ujumla kwa nchi nzima. Tulikuwa na migogoro zaidi ya 366 katika nchi nzima na tunaifanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, kuweka usuluhisho wa aina hiyo kwenye eneo moja tu la nchi, tunaomba sana Mheshimiwa Mbunge awe na subira tunalifanya kazi kwa nchi nzima. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wabunge na Madiwani ni wawakilishi wa wananchi lakini mara nyingi baadhi ya Wabunge na Madiwani wamekuwa wakitoa taarifa za migogoro kati ya wananchi kwenye maeneo yao lakini matokeo yake ile migogoro imageuzwa Wabunge au Madiwani wanaonekana ni wachochezî wanakamatwa na kuwekwa ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize Serikali, ni lini tabia hii itakoma Waheshimiwa Wabunge na Madiwani wanapotoa taarifa ioneckana kwamba taarifa hizo ni taarifa muhimu na za kufanyiwa kazi na ziheshimike? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini wakishaadhibiwa si wataacha hiyo tabia, sasa Mheshimiwa Waziri atajua lini wataacha?

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri, majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. GEORGE J. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani na Waheshimiwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, Vitongoji na Mitaa ni viongozi wa umma. Wanapotoa taarifa huwa zinapewa uzito unaostahili, isipokuwa tu kama kuna taarifa zingine ambazo zinakuja ku-*counter* kwamba labda wao wamehusika kwa njia moja au nyingine katika kusababisha mitafaruku illyojitokeza hapo ndiyo hatua nyingine huwa inachukuliwa. Hata hivyo, taarifa zao huwa zinachukuliwa kwa uzito unaostahili na kwa heshima kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sema tu kwamba wenzetu wa Jeshi la Polisi kupitia Sheria ya Kanuni ya Adhabu wanao uwezo wa kufanya *counter intelligence research* kujua kwa kina tatizo hasa ni nini. Sasa wanaweza wakamshikilia kiongozi kwa muda ili waweze kupata taarifa za ziada, lakini kwa kweli kama watazidisha muda ambao wanaruhusiwa kukaa na viongozi kwa ajili ya mashauriano hiyo itakuwa wanafanya kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali lake ni la msingi na kwa kweli tutaliangalia kwa umakini zaidi ili kusudi kuweza kuweka mazingira mazuri zaidi. Sheria ya Kumlinda Mtoa Taarifa ipo na ilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi wowote.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 512

**Barabara Inayounganisha
Mkoa wa Singida na Bandari ya Tanga**

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Mkoa wa Singida na Bandari ya Tanga inayoanzia Kijiji cha Unyankhanya kuititia Makyungu Misughaa – Chemba hadi Tanga ili kuchochea maendeleo ya Mkoa wa Singida?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makyungu – Chemba hadi Tanga inayoanzia Kijiji cha Unyankhanya ni sehemu ya mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Chemba – Kwamtoro hadi Singida yenye urefu wa kilometra 460 ambapo kazi ya upembizi yakinifu, usanifu wa kina pamoja na uandaaji wa nyaraka za zabuni iliyofanywa na Mhandisi Mshauri aitwaye *Inter-Consult Limited* ya Dar es Salaam ikishirikiana na Mhandisi Mshauri aitwaye *Consult Aurecon* kutoka Afrika Kusini ilikamilika mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuhudumia mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga eneo la Chongoleani,

Serikali itahakikisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca, swali la nyongeza.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii imechukua muda mrefu sana kukamilika kwa kiwango cha lami, na kwa kuwa tunayo Sheria ya *PPP*, ili kuacha kuendelea kutegemea zaidi bajeti, kwa nini Serikali imeshindwa kuweka msisitizo kwenye *PPP* ili kuhakikisha kwamba miradi hii pamoja na miradi ya ujenzi wa barabara inatekelezeka kwa wakati?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jesca Kishoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifahamishe tu Bunge lako Tukufu kwamba harakati za ujenzi wa barabara hii zimeshaanza, kwa sababu ujenzi wa barabara unaanza kwenye hatua ya usanifu, kupata michoro na tuko kwenye hatua ya kutafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu katika bajeti hii tutakayoanza mwezi wa Julai ya 2018/2019 tumetenga shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuanza ujenzi. Vilevile yapo mazungumzo ambayo yanaendelea ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua umuhimu wa hii barabara kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali imetupia macho na kwa kweli imeonyesha *commitment* ya hali ya juu kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilishwa. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Jesca Kishoa pamoja na hii *concept* ya *PPP*, tunakaribisha wadau wa *PPP* kama watajitokeza na kama mradi wao hautakuwa mzigo

kwa wananchi Serikali iko tayari kuchukua mawazo yake hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi hii. Umuhimu wa barabara ambayo imeulizwa katika swali hili inafanana kabisa na umuhimu wa barabara ya kutoka Haydom - Kidarafa - Mwanga - Nkhungi - Nduguti mpaka kwenye Daraja la Sibiti kwenda Simiyu. Ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu Mheshimiwa Kiula anafahamu kwa sababu muda si mrefu tulitembelea barabara hii kutoka Iguguno kupitia Gumanga, tukaenda mpaka Sibiti kuona maendeleo ya ujenzi wa daraja ambalo muda si mrefu litakamilika. Cha msingi niseme tu kwamba barabari hii ya Haydom – Kidarafa hatua zake za kuanza ujenzi ni nzuri na kama nilivyojibu siku chache zilizopita sasa tutakwenda kufanya mkutano wa wadau ikiwemo Waheshimiwa Wabunge na viongozi mbalimbali wa mikoa ambayo barabara hii itapita kwa sababu itaunganisha Mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Simiyu na mikoa mingine ile ya Kanda ya Ziwa. Kwa upande wa Serikali tuko katika hatua nzuri na wakati wowote tutaweza kuanza kujenga barabara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Kiula asiwe na wasiwasi. Najua tu barabara hii ikikamilika hiki kiungo cha hii barabara tena kutoka Singida kwenda Sibiti nayo ni muhimu ili kufupisha gharama za usafiri kutoka Singida kwenda kwenye Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maftah.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante. Wakati tunapitisha bajeti hapa nilzungumza juu ya barabara muhimu sana Kanda ya Kusini inayopita mikoa yote ya Kusini, kwa maana ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, barabara ya Ulinzi. Kwa kuwa bajeti haijasema chochote juu ya barabara hii kwamba imetengewa kiasi gani, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii ili huu mpaka wa Kusini unaoanzia Mtwara Mjini maeneo ya Mahurunga, Kitaya, Tangazo, Tandahimba, Newala mpaka kule Ruvuma uweze kulindwa sawasawa pale ambapo maadui wa nchi hii wanaweza wakatokea? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyezekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini maarufu kama *Gas City*, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, tunatambua umuhimu wa barabara hii ya ulinzi. Sisi kama Serikali ambacho tunakifanya kabla hatujaja kuboresha barabara iwe kiwango cha lami, tunahakikisha inapitika muda wote. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mtwara kwa ujumla tunahakikisha kwanza barabara hii inapitika lakini kwenye *strategic plan* zetu za Wizara tumeitazama. Labda tu akipata nafasi tuzungumze ili tuangalie tumeipanga lini tutakuwa kwenye hatua ya lami.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa sasa hivi msukumo mkubwa ilikuwa ni kuhakikisha hii barabara inayotoka Mtwara Mjini - Mnivata - Tandahimba - Newala - Masasi inakamilika kwa kiwango cha lami. Ukiwa Tandahimba iko barabara inakwenda kuungana na barabara hii ya msingi, lakini kama alivyosema ukiwa Newala kiko kipande kinakwenda kuungana na barabara hii, kwa hiyo, barabara hii kubwa ikikamilika basi tutaweza kuzingatia na hii barabara ya msingi

kuhakikisha inajengwa kwa kiwango cha lami. Tuonane tuangalie kwenye mipango ya Wizara ni lini tutakwenda kwenye hatua ya lami.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki sasa aulize swali lake.

Na. 513

**Ujenzi wa Barabara ya Bigwa –
Kisaki kwa Kiwango cha Lami**

MHE. OMARY T. MGUMBA aliuliza:-

Barabara ya Bigwa – Kisaki ni muhimu kiutawala na kiuchumi kwa kuwa inaunganisha Mbuga ya Selous, Mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara:-

(a) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

(b) Nyumba za wakazi zilizopo pembezoni mwa barabara hiyo zimebekwa alama ya X kwa muda mrefu lakini wananchi hawajalipwa fidia. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi hao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kujengwa kwa kiwango cha lami barabara ya Bigwa – Kisaki kwa kuanza na kipande cha barabara ya kuanzia Bigwa - Mvuha chenye urefu wa kilometra 78. Mhandisi Mshauri alitoa Ripoti ya Awali (*Draft Final Report*) tangu tarehe 2 Julai, 2017. Kazi hii imefanywa na Kampuni ya *Unitec Civil Consultants Limited* ya Dar-es-Salaam ikishirikiana na Kampuni ya *Mult-Tech Consultant Limited* kutoka Gabone, nchini Botswana. Kwa sasa Mhandisi Mshauri anaendelea kufanya marekebisho mbalimbali yaliyoelekezwa na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) ili kukamilisha kazi hiyo ya usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya usanifu wa barabara hii kukamilika na gharama kujulikana, Serikali itatafuta fedha ili ujenzi uanzwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Serikali italipa fidia kwa wananchi ambao nyumba zao zitaathirika na ujenzi wa barabara ya Bigwa – Mvuha – Kisaki zilizowekwa alama ya X kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mgumba, swali la nyongeza.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, hayo marekebisho anayoyasema Mheshimiwa Waziri yalishafanyika tangu mwaka jana na sasa hivi tuko kwenye hatua ya kusubiri fedha kama anavyosema. Kwa kuwa barabara hii umuhimu wake umeongezeka kitaifa kwa sababu mradi wa kufua umeme wa *Stiegler's unaojengwa utatumia* barabara hii lakini pia mpango wa Serikali wa kufufua utalii katika Ukanda wa Kusini hasa katika Mbuga ya Selous barabara hii itahitajika. Je, Serikali haioni umuhimu wa

kuharakisha ujenzi wa barabara hii ili kufungua utalii katika ukanda wa Kusini katika Mbuga ya Selous ukizingatia zaidi ya 70% ya mbuga hii iko Mkoa wa Morogoro? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa, Sheria Tathmini inasema kwamba mtu akishafanyiwa tathmini alipwe ndani ya miezi sita na Serikali sasa inasema kwamba itajenga barabara hii kwa kutegemea upatikanaji wa fedha. Kwa kuwa malipo ya fidia yanalipwa baada ya fedha kupatikana, je, Serikali inatoa kauli gani kwa watu watakaoathirika na mradi huu ambao hawafanyi maendelezo ya nyumba zao zaidi ya miaka nane sasa ili waweze kuendelea na ujenzi wao mpaka hapo hizo hela zitakapopatikana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Mgumba kwa sababu amefuatilia sana barabara hii. Tangu niingie kwenye Bunge hili kila wakati nimemsikia akizungumza juu ya barabara ya Bigwa – Kisaki. Hata Waswahili wanasema baada ya dhiki ni faraja, ni faraja kwamba sasa tunaenda kutengeneza hii barabara na hatua iliyofikia siyo haba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la kwanza, amezungumza juu ya umuhimu wa barabara hii kujengwa kwa haraka. Kweli maeneo haya ni muhimu sana kwa sababu barabara ya Bigwa – Kisaki ita-*facilitate* upitishaji wa mizigo na vitu muhimu kwenda kwenye ujenzi sehemu tunayoenda kufua umeme kule *Stiegler's Gorge*, lakini pia naya fahamu maeneo haya yana utalii kama alivyosema na eneo hili pia ni muhimu sana kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeitazama barabara hii tumeitazama na hatua iliyofikiwa siyo hatua mbaya, kipande cha kilometa 78 tutakwenda kuungana na barabara inayotoka Ngerengere ambayo ndio tumeipa kipaumbele zaidi ili mizigo ianze kupita Ngerengere kwenda Mvuha mpaka Stiegler's Gorge. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi barabara zote hizi mbili zitaunganika tu, tukianza na ile ya Ngerengere pamoja na hii aliyozungumza. Barabara zote ziko katika maeneo yake nasi tumejipanga kuhakikisha tunaendelea kujenga kwa kiwango cha lami. Hatua iliyofikiwa ni nzuri ya kutafuta fedha ili tuenze ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa eneo hili la Morogoro kwa ujumla wawe na subira wakati tunaendelea na harakati hizi. Hata kwa mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 5 kuanza kujenga barabaa hii ya Ngerengere - Mvuha, kwa hiyo, kuja kuunganisha na barabara hii itakuwa rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia utaratibu na kanuni zipo kwamba totalipa fedha kulingana na thamani ya fedha kwa wakati huo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mgumba na wananchi wake ambao wamepisha maeneo kwa muda mrefu, niwapongeze sana, wamevumilia miaka nane, tunaendelea kutafuta fedha ili tulipe fidia hii. Totalipa fidia hii kulingana na kanuni na sheria zinavyosema ili tuweze kuwa-*compensate* wananchi hawa kwa sababu wamesubiria fidia yao kwa muda mrefu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swalii moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu vizuri sana Mpwapwa na barabara ya kutoka Kongwa - Mpwapwa anaifahamu vizuri sana; na kwa kuwa Serikali imekubali kujenga barabara ya lami kutoka

Kongwa - Mpwapwa, je, barabara hii kama nilivyoomba itaanza Mpwapwa - Kongwa? Naomba Waziri awathibitishie hilo wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa au ye ye anasemaje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwei Mheshimiwa Lubeleje amekuwa akifuatilia sana barabara hii. Wiki kama nne zimepita baada ya mvua kupungua nilitembelea eneo la Mpwapwa nimeenda kuona hata eneo la Godegode ambalo amekuwa akipigia kelele sana ili tuje na utaratibu wa kuhakikisha turekebisha barabara iweze kuitikika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu barabara hii ya lami inayotokea barabara kuu kwenda Kongwa ujenzi unaendelea vizuri, hii ndiyo sehemu ya barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge anazungumza. Nafahamu *concern* yake ni kuhakikisha tunajenga ile barabara ya kutoka Mpwapwa Mjini ili ije ikutane na hii barabara inayotoka Kongwa na tumetenga fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Lubeleje juhudhi zake zinazaa matunda na anafanya kazi nzuri na wananchi wa Mpwapwa watambue hivyo kwamba tutaendelea kujenga barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jana tulipiga hesabu kidogo kuona kwamba kwa kiasi cha fedha ambacho tumetenga tunaweza sasa tukawa na utaratibu wa mkataba wa kilometra karibu 7 hivi tukaanza kujenga kutoka Mpwapwa Mjini. Kwa hiyo, tutakwenda hatua kwa hatua kadiri fedha zinavyopatikana kuhakikisha eneo lake lote hili linapata barabara ya lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Lubeleje asiwe na wasiwasi .

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mzumbe – Mgeta ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko utaratibu wa kuratibu ahadi zote za viongozi wetu wakuu kuhusu ujenzi wa miundombinu hii ya barabara. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia barabara hii ya Mgeta, tutaitazama kadiri itakavyowezekana tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. Nilikuwa nimepata kabrasha kwa maana ya kuziangalia ahadi zote za viongozi kuanzia Awamu zilizopita mpaka sasa hivi, labda hata baadaye tunaweza tukazungumza ili tuone tumejipanga vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fursa zimekuwa nzuri kwa kuwa zile harakati za kuunganisha mikoa hatua iliyofikiwa ni nzuri sasa tutakwenda kuunganisha wilaya na mikoa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira lakini tutazungumza ili tuione sasa kwenye *strategic plan* yetu kwamba barabara hii tumeipangia nini. Muhimu zaidi ni kuhakikisha kwamba ahadi zote ambazo viongozi wakuu wamezitoa na sisi kama Wizara tunazitekeleza ili kutekeleza ahadi za viongozi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka, swali fupi la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mji wa Tunduma ni wa kibashara na kuna mpaka ambao unatumwa na nchi karibu nane za Kusini na Kati mwa Afrika. Kumekuwa na msongamano mkubwa sana wa malori yanayovuka mpaka ule na kusababisha wananchi wa Tunduma kuchelewa kufanya shughuli zao kwa sababu ya msongamano ule. Kuna barabara ya kilometra 12 kutoka eneo la Mpemba kuja Tunduma Transfoma ambapo viongozi wengi wameahidi kuijenga kwa kiwango cha lami ili kupunguza msongamano kwa magari yanayotoka Sumbawanga kwenda Mbeya na yanayotoka Mbeya kwenda Sumbawanga lakini pia kuwarahisishia usafiri wananchi wa Mji wa Tunduma. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kama ahadi za viongozi zilivyotolewa? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua ziko *challenge* kubwa za msongamano wa magari kwa sababu Mji wa Tunduma unakua kwa kasi na huduma za kijamii zimeongezeka sana. Nimhakikishie Mheshimiwa Mwakajoka na wananchi wa Tunduma kwamba tumejipanga vizuri kuhakikisha maeneo yote ambayo yana changamoto za msongamano tunayashughulikia, kwa hiyo, nimtoe hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijafanya ziara Mkoa wa Songwe, baada ya Bunge hili nitatembelea huko, nafikiri itatupa nafasi zaidi tuweze kuzungumza na niweze kuona. Pia niiione mipango iliyoko *TANROADS* Mkoa kuhusu maboresho ya eneo hili la Tunduma ili tuweze kuondoa shida ambazo zinawapata wananchi na kuondoa tatizo la kupoteza muda kwa ajili ya kwenda kuzalisha katika maeneo mbalimbali.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 514

Kuongezeka kwa Wagonjwa wa Figo Nchini

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Moja kati ya matatizo makubwa yanayoikabili nchi yetu ni maradhi ya figo na idadi ya wagonjwa wa figo inazidi kuongezeka siku hadi siku:-

(a) Je, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili hupokea wagonjwa wangapi kwa siku?

(b) Je, Serikali ipo tayari kutoa elimu kwa umma juu ya chanzo cha ugonjwa huo na namna ya kujikinga?

MWENYEKITI: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 wakati wa huduma za utakasaji wa damu kwa wagonjwa wa figo zilipoanzishwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kulikuwa na wagonjwa wa figo chini ya 10 waliokuwa wakihitaji huduma hii, lakini kwa sasa tuna wagonjwa 240 waliopo kwenye huduma hii. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inatoa huduma ya utakasaji damu kila siku isipokuwa siku ya Jumapili

na kuna jumla ya vitanda 42 vya kutolea huduma ambapo kwa siku wanahudumiwa wastani wa wagonjwa 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kiliniki ya wagonjwa wa figo ambayo inafanyika kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imekuwa ikiona wastani wa wagonjwa wapatao 60 kwa siku. Sanjari na hilo, Serikali kupitia hospitali zake za kibingwa imefanikiwa kuanzisha huduma za kupandikiza figo ambapo jumla ya wagonjwa 10 wameshapata huduma hiyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na mgonjwa mmoja katika Hospitali ya Benjamin Mkapa na upandikizaji huu utaendelea kwa wagonjwa watano kila mwezi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na wakati huohuo Hospitali ya Benjamin Mkapa ikiendelea kujengewa uwezo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Chama cha Wataalam wa Magonjwa ya Figo Tanzania tunaendelea na jitihada za kutoa elimu za kujikinga na madhara ya magonjwa ya figo kwa kuzingatia kanuni za afya na kupima mapema ili kutambua na kupata matibabu kwa wakati. Elimu juu ya uelewa wa madhara yatokanayo na matumizi ya vileo, lishe isiyozingatia misingi ya afya bora na kutofanya mazoezi vinaweza kusaidia sana kuzuia magonjwa ya figo. Elimu hii imekuwa ikitolewa kupitia vyombo vya habari, ikiwemo makala kwenye magazeti, vipindi vya runinga na redio, vipeperushi, utoaji wa elimu za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na pia kwenye kampeni mbalimbali za magonjwa yasiyoambukiza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia Shomar, maswali ya nyongeza.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali la kwanza, kwa kuwa maradhi ya figo ni hatari sana. Je, Mheshimiwa Waziri atawasaidia viyi wananchi wanaoishi vijijini ili kujitambua mapema kwamba tayari wameshaambukizwa na maradhi hayo na wakati huo baadhi yetu hatupendi ku-*check* afya zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna baadhi watoto wachanga huzaliwa na maradhi ya figo wakati wazazi wao hawatambui watoto kuwa na maradhi hayo na kupelekeea mtoto kusononeka. Je, Wizara inatoa elimu gani kwa wazazi baada ya kuzaa ili kuwa na hofu ya maradhi hayo kwa watoto wao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli magonjwa ya figo yanazidi kuongezeka na hoja yake ya msingi illkuwa, je, wale watu ambao wako vijijini wanawezaje kutambua magonjwa haya. Niendelee kusisitiza kwamba magonjwa haya ya figo visababishi vikubwa sana kwanza ni ugonjwa wa kisukari lakini la pili ni ugonjwa wa shinikizo la damu. Tunaweza tukazuia magonjwa haya tukizingatia mambo makubwa matatu. La kwanza ni kuhakikisha kwamba tunapata lishe bora badala ya bora lishe. Pili, kujenga utaratibu wa kufanya mazoezi lakini la tatu ni kuhakikisha tunakuwa na matumizi sahihi na yasiyopitiliza kiwango ya pombe na sigara. Kwa hiyo, niendelee kuhamasisha kwamba tuendelee na utamaduni wa kufanya *check-up* ya miili yetu mara kwa mara na iwapo tutafanya hivi, tunaweza tukayagundua magonjwa haya mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameulizia kwa watoto wachanga. Watoto wachanga nao wanaweza wakapata magonjwa ya figo kwa sababu ya maumbile ya figo zao kumekuwa na changamoto wanaweza wakazaliwa na tatizo la figo. Dalili gani ambazo mtu anaweza akazigundua kama mtoto anaweza kuwa na tatizo la figo? Mara nyingi mtoto anakuwa anavimba macho, sura, tumbo, miguu na sehemu mbalimbali za mwili. Mara nyingi unakuta hata ile haja ndogo haipati kwa kiwango kinachostahili.

Niendelee kusitiza kwamba iwapo mtu ataona mtoto ana dalili kama hizo afike katika vituo vya afya aweze kupata ushauri sahihi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasna Mwilima na Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wagonjwa wa figo wako pia kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini. Kwa vile wanapokuwa na matatizo hayo wanatakiwa waende hospitali ya wilaya ili waweze kupata *referral* ya kwenda Hospitali ya Muhimbili. Je, ni lini sasa Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Jimbo la Kigoma Kusini ili wagonjwa wangu wa vijijini wenye ugonjwa wa figo waweze kupata eneo la kutibiwa na kupata *referral* ya kwenda Muhimbili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunaendelea kuboresha mifumo yetu ya rufaa na huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na za magonjwa haya ya figo. Sasa hivi huduma hizi kwa kiasi kikubwa sana tumeweza kuzisambaza sehemu mbalimbali za nchi, tunazijengea uwezo hospitali zetu za rufaa za mikoa vilevile tunazijengea uwezo hospitali zetu za wilaya kuweza kutambua dalili za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, magonjwa haya ya figo yanababishwa sana na magonjwa makubwa mawili ya kisukari na shinikizo la damu ambayo kama hatutaweza kuyadhibiti vizuri na

kupata matibabu yaliyo sahihi yanapelekea mtu kupata ugonjwa wa figo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba swalii la msingi la Mheshimiwa Hasna Mwilima alikuwa anaulizia ni lini sasa Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya katika Jimbo lake la Kigoma Kusini ili wananchi wake wawewe kupata huduma hii. Katika bajeti hii ya mwaka huu Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 67 za wilaya. Naamini hospitali ya wilaya hii itakuwa ni moja kati ya hospitali hizo zitakazojengwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema na mimi najua kwamba ugonjwa wa kisukari ndiyo unaoongoza katika magonjwa yasiyoambukiza na mimi mwenyewe ni muathirika. Wataalam wanasema ugonjwa huu hauna dawa hasa *Diabetic 1* lakini wataalam wengine hasa wa tiba mbadala wamekuwa wakidai kwamba ugonjwa huu unatibika. Ndiyo maana wengi wamekuwa wakienda huko ama wanatibiwa kweli au hawatibiwi. Naomba kujua Serikali inasema nini kuhusiana na hizi tiba asilia ambazo kimsingi naona kama zinapotosha. Nilikuwa naomba kauli ya Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeza kwa kuwa ni mfuatiliaji mzuri sana masuala ya magonjwa yasiyoambukiza hususan ugonjwa huu wa kisukari. Hoja yake ya msingi amegusia suala la tiba asili ya magonjwa ya kisukari. Naomba nitoe kauli kwamba hadi hivi sasa hatuna dawa yoyote ya

tiba asili ambayo sisi kama Serikali tumeithibitisha kwamba inatibu ugonjwa wa kisukari. Nitumie nafasi hii kuwaambia watoa tiba za asili kwamba tunawahitaji na tunawataka wajisajili kama watoa huduma lakini kama kuna mtu ambaye anadhani ana tiba/dawa inayoweza kusaidia katika magonjwa yoyote yale kuna utaratibu wa kuhakikisha dawa hiyo inafanyiwa utafiti na inasajiliwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba mpaka sasa hatuna dawa ambayo inatibu ugonjwa wa kisukari.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza.

Na. 515

NIMR kuanzisha Chuo Kikuu

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) imekuwa na mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Mafunzo yanayohusiana na tafiti hizo maeneo ya Amani Muheza:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza azma hiyo?
- (b) Kama Serikali haipo tayari, je, itakuwa tayari kukabidhi majengo yaliyopo Amani - NIMR kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inayosimamia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*National Institute of Medical Research*) kwa maana ya *NIMR* Act 2002, Cap 59, haiipi mamlaka ya kuanzisha au kutoa shahada lakini inaruhusu utoaji wa mafunzo mafupi na elimu kwenye maeneo yanayohusiana na tafiti za kiafya. Wizara kuititia *NIMR* inalenga kusimamia utekelezaji wa jukumu hili la msingi kwa taasisi kwa kuanzisha mafunzo mafupi yatakayoendana na mamlaka na majukumu ya taasisi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa taasisi haipo tayari kukabidhi majengo yaliyomo *NIMR* Amani kwa Halmashauri ya Wilaya na Muheza, kwa kuwa Wizara kwa kuititia *NIMR* ina mpango wa kuyatumia majengo hayo ikiwemo majengo ya ofisi, karakana, maabara, hosteli na watumishi waliobobea katika nyanja mbalimbali kutoa mafunzo ya muda mfupi kwenye eneo la tafiti za afya ili kuwajengea uwezo wataalamu katika sekta ya afya nchini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi Adadi.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayaendani na hali halisi iliyopo Amani kule taasisi kwenyewe (*NIMR*) ambapo majengo hayo yapo. Mheshimiwa Waziri wa Afya alifika kule na aliyaona majengo yale na baada ya kuongea na wananchi aliahidi kwamba angeweza kuleta shilingi billioni 2 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba chuo kikuu kile kinaanza kujengwa au majengo yale yanaanza kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIMR* ya Tanzania ina sifa kubwa sana duniani kutokana na utafiti inaoufanya. Kwa sababu majengo yale yamekaa muda mrefu na kugeuka kuwa magofu, kuna mpango gani wa haraka wa kuweza kuyanusuru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, hata kama sheria hairuhusu kuanzisha chuo kikuu lakini inaweza kubadilishwa kwani majengo yale yana *facilities* zote za kuanzisha hicho chuo kikuu. Kwa kuanzia ni lini mtaanza kutoa hayo mafunzo ya vyeti pamoja na diploma ili kuweza kuokoa hali ya pale ilivyo? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana amekuwa akifuatilia suala hili la vituo vyetu vya utafiti vya Amani pale Muheza. Niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto alipita pale na hilo tunalikiri na aliahidi kwamba majengo yale yatafanyiwa ukarabati. Niendelee kusisitiza kwamba ahadi hiyo bado ipo na sisi kama Serikali tunaendelea kujipanga kutafuta fedha ili kuyafanya ukarabati majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi taasisi yetu hii ya *NIMR* tunaendelea kuijengea uwezo. Tulipokuwa tumelanzisha mwanzoni makusudio yalikuwa ni kuelekeza nguvu zaidi katika magonjwa ya kuambukiza lakini sasa hivi kumekuwa na mabadiliko makubwa sana katika magonjwa yasiyoambukiza na tumeanza kuona tunakuwa na magonjwa haya. Kwa hiyo, tumewaelekeza *NIMR*vilevile kuanza kujikita katika kufanya utafiti katika magonjwa yasiyoambukizwa. Kwa hiyo, tutapokuwa tumefanya ukarabati huo tutajaribu sasa kuhakikisha kwamba pamoja na hizi tafiti ambazo tumekuwa tunazifanya katika magonjwa ya kuambukiza vilevile tunaanzisha utaratibu wa utafiti kwa magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Sheria ya *NIMR*hairuhusu sisi kuanzisha chuo

kikuu lakini haituzuii kufanya kazi na baadhi ya vyuo vikuu kwa kujenga ushirikiano wa kufanya tafiti (*research*). Katika swali lake ameuliza ni lini tutaanza sasa kutoa yale mafunzo ya muda mfupi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kujipanga na katika mwaka wa fedha ujao tunatarajia kwamba tutaanza kutoa mafunzo mafupi mafupi katika kada mbalimbali za afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib, swali fupi la nyongeza.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri amenitosheleza, nilichotaka kukiuliza amekijibu *automatic*. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 516

Tatizo la Wanyama Waharibifu – Bukoba Vijijiini

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI aliuliza:-

Wananchi wa Bukoba Vijijiini wanakabiliwa na tatizo kubwa la wanyama waharibifu kama vile ngedere na kadhalika na wanyama hao sasa wanavamia vijiji na kusababisha madhara kwa wananchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuwanusuru wananchi wa Bukoba Vijijiini na balaa la wanyama hao waharibifu?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba njibui swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinairy Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua uwepo wa tatizo la wanyamapor wakali na waharibifu linalojitokeza katika wilaya zaidi ya 80 hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Bukoba Vijijiini. Wanyamapor wanaoleta usumbufu kwa wananchi katika wilaya hiyo ni tembo, mamba na ngedere. Tembo kutoka kwenye Ranchi za Kagoma na Mabale wamekuwa wakivamia maeneo ya mashamba na makazi ya wananchi jirani na ranchi hizo. Aidha, mamba wamekuwa wakijeruhi wananchi pembezoni mwa Ziwa Viktoria hususan maeneo ya Kemondo. Vilevile ngedere wanasumbua wananchi kutoka kwenye misitu ya asili ya Kizi, Bugando, Katangara, Kereuyangereko, Kemondo na Rasina. Misitu hiyo ipo kwenye Kata za Katoma, Karabagaine, Bujogo na Kishongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imechukua hatua za kudhibiti tatizo hilo kwa kufanya doria ambapo Askari wa Wanyamapor kutoka Kikosi Dhidi ya Ujangili - Mwanza na Pori la Akiba Biharamulo - Burigi - Kimisi (*BBK*) wakishirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijiini ambapo waliua jumla ya ngedere 103 na kufukuza makundi kadhaa. Doria hizo zilifanyika katika Kata za kemondo, Katerero, Kanyengereko, Maruku, Katoma, Bujogo, Karabagaine, Nyakato, Kikomela, Ibwela, Nyakibimbili, Kaibanjara, Buterankunzi, Mikoni, Kyamlaille, Lubafu, Kagya, Lukoma, Ruhunga, Buhendangobo na Kishanje. Sambamba na doria hizo, elimu kuhusu mbini za kujiepusha na kujihami na wanyamapor wakali na waharibifu imetolewa katika kata 21 ka kushirikiana na Maafisa Ugani. Wananchi wameelekezwa mbini rafiki za kuwafukuza na kuwadhibiti wanyamapor hao wakiwemo ngedere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua uhaba wa Askari wa Wanyamapor katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijiini hivyo itaendelea kushirikiana na halmashauri husika katika kudhibiti wanyamapor wakali na

waharibifu ili wasilete madhara kwa maisha na mali za wananchi. Hata hivyo, naomba nitoe rai kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijiji ni kuajiri Askari wa Wanyamapori kwa ajili ya kuharakisha udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kahigi, swali la nyongeza.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali iko pamoja na Halmashauri ya Wilaya kudhibiti wanyama hawa waharibifu, je, Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha kuwa inawapatia vifaa vya kutosha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunaelewa kuwa wanyama hawa ni waharibifu, je, hakuna njia nyingine ya kuwadhibiti wanyama hawa badala ya kuwauwa? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akishirikiana na Serikali katika kufuatilia masuala haya. Niseme tu kama nilivyokuwa nimesema kwenye swali la msingi, tumechukua hatua kadhaa katika kuhakikisha tunawadhibiti wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo ipo, ni kweli kabisa vifaa vya kudhibiti bado havitoshi hata hivyo tunaendelea kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunapata vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kuwadhibiti wanyamapori

wakali na waharibifu katika maeneo yote ikiwa ni pamoja na kutumia zile ndege zisizowakuwa na rubani lakini pia kufanya shughuli nyingine ambazo zitawafukuza wale wanyamapori kusudi wasiletie ucharibifu ule ambao umekuwa ukijitokeza katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kweli kabisa hatupendekezi na hatushauri watu kuwaua wanyamapori, kwa sababu wanyamapori wanayo haki ya kuishi katika nchi hii kama Mungu alivyofanya uumbaji yeye mwenyewe kwamba lazima viwepo hapa duniani. Kwa hiyo, hizi ni maliasili ambazo lazima zilindwe. Hata hivyo, pale inapoonekana kwamba wamekuwa wengi tunafanya uvunaji endelevu ndipo hapo tunaweza kuwaua. Ngedere wakizidi ndiyo tunawaua *otherwise* tunakuwa na idadi ambayo lazima iendelee kuwepo na hatushauri viongozi wetu au wafanyakazi wetu kuwaua wanyama hao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi katika Wilaya ya Urambo wanateseka kutokana na migogoro iliyopo kwenye mapori ya hifadhi. Nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri ambaye anajibu maswali sasa hivi alikuja kumaliza migogoro ile lakini haikuwezekana kutokana na muda mfupi uliokuwepo. Je, anatuambia nini sisi wananchi wa Urambo atakuja kumaliza migogoro iliyopo Runyeta ambako walichomewa nyumba zao na mazao yao, Tevera katika Kata ya Uyumbu na Ukondamoyo ambayo bado kuna mchuano mkubwa sana ambapo wananchi wamekosa mahali pa kulima kutokana na migogoro ya misitu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Margaret Sitta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amefanya kazi nzuri ya kuhamasisha wadau mbalimbali kuhakikisha fedha zinapatikana kwa ajili ya ujenzi wa vyoo katika shule zetu. Hongera sana mama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nilishafika katika eneo lile, nilikutana na wananchi na tukajadiliana juu ya mgogoro uliopo na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atatembelea eneo lile ili aweze kukutana na wananchi na kuhakikisha kwamba sasa ule mgogoro ambaa ulikuwepo muda mrefu unaisha mara moja. Kwa hiyo, naomba asubiri kidogo Waziri ataenda katika eneo hilo na sasa wataaka pamoa kulitafutia uvumbuzi wa kudumu tatizo hilo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Issaay.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mwaka 2015/2016 wanyama wakali walipoteza maisha ya wananchi watano katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Hivi sasa Halmashauri ya Mbulu toka ianzishwe mwaka 2015 haina Maafisa wa Wanyamapor. Je, ni lini Serikali yetu itatusaidia kutupatia Askari wa Wanyamapor katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na upungufu wa wafanyakazi katika maeneo mengi ikiwemo Maafisa Wanyamapor. Katika jitihada ambazo zinafanyika sasa hivi tumeweka kwenye bajeti inayokuja kuangalia kama tunaweza kupata wafanyakazi wachache ambaa

tutawasambaza katika wilaya mbalimbali hapa nchini. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira hilo likikamilika tutafikiria Wilaya ya Mbulu ili waweze kupata wafanyakazi hao.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 517

**Migogoro ya Mipaka kwenye
Vijiji vinavyopakana na Hifadhi**

MHE. JOSEPH L. HAULE aliuliza:-

Kumekuwa na migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na wananchi kwenye vijiji vinavyopakana na Hifadhi hizo kama vile Ruhembe, Kitete, Kikwalaza, Mji Mpya, Ihambwe, Mululu na sasa Kitongoji cha Lugawilo, Kata ya Uleling'ombe:-

Je, ni lini Serikali itaweka mipaka ili wananchi hao wasiendelee kunyang'anjywa ardhi yao kwa kisingizio cha kuwa wameingia kwenye Hifadhi?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hakuna mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Mikumi na Vijiji vya Ruhembe na Ihambwe wala na Vitongoji vya Kikwalaza na Mji mpya ambavyo vimepakana na Hifadhi ya Taifa Mikumi. Mgogoro uliokuwepo ulishughulikiwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kilosa, Viongozi wa Hifadhi, Viongozi wa Vijiji na wajumbe wanne

kutoka kila kijiji. Uhakiki wa mpaka wakati wa usuluhishi wa migogoro hiyo ulisimamiwa na viongozi wa Ardhi wa Mji Mdogo Mikumi, wataalam wa Ardhi Wilaya ya Kilosa, Mshauri wa Ardhi Mkoa wa Morogoro na wataalamu wa mipaka wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kufuatia utatuzi huo, eneo la mpaka unaotenganisha vijiji na hifadhi, ulifwekwa na vizingi vya kudumu (*beacons*) kuwekwa pamoja na vibao vya kuonesha mpaka wa hifadhi katika baadhi ya maeneo. Vilevile hifadhi imeendelea kusafisha mpaka wake na vijiji vyote kila Mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Mikumi haina mgogoro wa mpaka na Kijiji cha Kitete Msindazi, kwani mpaka uliobainishwa na Tangazo la Serikali Na.121 la mwaka 1975 ultafsiriwa ardhini kwa usahihi na wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambapo uliridhiwa na pande zote husika zilishirikishwa katika uhakiki wa mpaka huo amba ni viongozi wa vijiji na Hifadhi ya Mikumi chini ya usimamizi ya Kamati ya Ulinzi wa Usalama ya Wilaya ya Kilosa. Hata hivyo, lipo eneo la ardhi (*general land*) ambalo siyo sehemu ya hifadhi wala kijiji kati ya mpaka wa hifadhi na Kijiji cha Kitete Msindazi. Kisheria eneo hilo liko chini wa Kamishna wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Mikumi na Kitongoji cha Lugawilo, Kata ya Uleling'ombe kwa kuwa hifadhi haipakani na kijiji chochote cha Kata ya Uleling'ombe. Aidha, naomba Mheshimiwa Mbunge atakapopata nafasi atembelee Hifadhi ya Taifa Mikumi kupata uhalisia wa kile kinachofanyika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haule, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kufanya ziara Jimboni kwangu Mikumi, pindi ambapo simba walivamia zizi la mwanakijiji wetu pale Kikwalaza na akaweza kuzungumza na wananchi. Pia alifanikiwa kwenda Ruhembe, bahati mbaya sana ni

kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri hakuwasiliza wananchi bali alisikiliza haya ambayo anaambiwa na viongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza niseme tu, kama kweli tunaipenda nchi yetu, sisi tunajua kwamba kuwa na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi siyo laana bali ni baraka kutoka kwa Mungu, lakini ukweli ni kwamba wananchi wa Kata ya Ruhembe, Kijiji cha Kitete Msindazi na Kielezo wanateseka sana kwa sababu ya kunyimwa haki zao za msingi za kuishi maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na ziara aliyoifanya, yale yote aliyoayazungumza kule hakuna hata kimoja kilichotekelawa. Nimwombe asiwasikilize hawa wanaomwandikia hivi vitu, aje awasikilize wananchi wa Kata wa Ruhembe wamwambie A, B, C na vitu vingine vyote. Kwa hiyo, hiyo ndiyo rai yangu kwake kwamba namkaribisha tena Mikumi, azungumze na wananchi hawa viongozi wanaomwambia yote yamekamilika na kwamba kuna amani, wanafanyakazi yake iwe ngumu sana kwa kutokuwa na amani katika Kata yetu na Jimbo la Mikumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sasa hivi wananchi wa Mikumi, napata ukakasi kusema kama wanapotea au wanachukuliwa na watu wasiojulikana, kuna watu wanatoka Usalama na TANAPA wananchi wa Mikumi wanakufa na wanapotea na wengine wanarudi wakiwa vilema kwa sababu tu wanaonekana kuchukuliwa katika hali ambayo haipo na tukiwatafuta katika Vituo vya Polisi hatuwapati, tunaambiwa wamepelekwa Dar es Salaam. Je, Serikali inasemaje kuhusu wananchi wa Mikumi wanaopotea? Mpaka sasa takribani wananchi 40 kutoka Kata za Muhenda, Ruhembe, Kidodi wamepotea hatujui wako wapi. Serikali inataka kutuambia nini kuhusu hawa ndugu zetu? Tumechoka kuzika nguo na ndugu zetu hatuwaoni? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza lilikuwa ni rai tu, kwa hiyo, jibu swali la pili.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nimeshatembelea eneo hilo na ni kweli kabisa nilikaa na wananchi tukaweza kuzungumza na wakabainisha mambo mengi na tuliyawekea mkakati wa namna ya kuyatatu. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kipindi kati ya sasa na mwezi Septemba, tena wakati nakwenda Kilombero, nitapita kwenye eneo hilo ili tuweze kukutana na hao wananchi ili tuone kama kweli matatizo yao yanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hao wananchi ambao anasema kwamba wanapotea bila sisi kujuu, nadhani hizi taarifa kama Serikali hatunazo. Kama Mheshimiwa Mbunge anayo majina na anasema wananchi karibu 40 wote wamepotea, nadhani ni wakati muafaka tupatia hayo majina ili nasi Serikali tuweze kushirikiana na wananchi kubaini hao wananchi wote watakuwa wamekwenda wapi. Ni msimamo wetu kama Serikali kwamba kazi yetu ni kulinda wananchi na kuhakikisha wanaendelea kuishi vizuri na kufanya shughuli zao.

MENYEKITI: Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili ndani ya Jimbo la Mlimba wamepeleka barua kwamba wananchi wakulima na wafugaji mwezi Julai waondoke wakati wa mipaka ya bonde hilo hajjafanyiwa kazi na Waziri aliunda timu, kwenda kurekebisha mipaka ya *Ramsar*. Nini kauli ya Serikali kuhusu vitisho kwa wananchi hawa ambaa hata mazao yao hawajavuna?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Kiwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mnamo mwaka jana tulitembelea bonde lote na tukazungumza na wananchi. Wananchi waliomba badala ya kuhamza katika kipindi kile wapatiwe muda wa kutosha wa kuijandaa na waweze kuvuna mazao yao ndipo wahame. Ndipo Serikali ikatoa agizo kwamba ifikapo mwisho wa mwezi Agosti, 2018 wananchi hao wote wawe wamehama na wamevuna mazao yao yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kama unaniambia kwamba wameambiwa wahame mwezi wa Julai, ni kinyume na agizo tulilokuwa tumelitoa awali. Agizo la Serikali tulisema wananchi wale waachwe, wavune mazao yao lakini ikifika tarehe 31 Agosti, 2018, wananchi wote wawe wameshahama katika eneo hilo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Susan na wananchi wake waendelee kutulia, wavune kwa utaratibu ili kusudi wahamie katika yale maeneo ambayo watakuwa wameelekezwa na Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malocha, swali fupi la nyongeza.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Ni lini Serikali itatatua mgogoro wa muda mrefu wa mpaka kati ya Hifadhi ya Uwanda na Vijiji vya Ilambo, Mpande, Kilangawana, Legeza, Kapenta, Mkusi na Iwelamvua ili kuondoa manyanyaso ambayo wananchi wanapata kwa kunyang'anywa mazao, vifaa vyao vya kilimo na kuwapiga na mwaka juzi mtu mmoja aliuwawa? Ni lini Serikali itatatua mgogoro huu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Malocha, Mbunge machachari kweli kweli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kumekuwepo na changamoto ya mgogoro ambayo imekuwepo katika eneo lile. Hivi sasa tumejipanga katika kipindi hiki, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atakwenda kuona eneo hilo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili kusudi apate ratiba kamili ni lini atakuja, mtatembalea maeneo ya vijiji vyote hivyo na kuona ni hatua gani zichukuliwe kuhakikisha kwamba hiyo migogoro ambayo imedumu muda mrefu basi yote inatatuliwa kwa kipindi hiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara yetu ya mwisho, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete aulize swalii lake.

Na. 518

Hitaji la Kiwanda cha Maziwa – Busokelo

MHE. FREDY A. MWAKIBETE aliuliza:-

Busokelo ni mionganini mwa Halmashauri zinazozalisha maziwa ya ng'ombe kwa wingi ambapo kwa mwaka inazalisha zaidi ya litu milioni 50:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia kumalizia Kiwanda cha Maziwa kinacho jengwa Kata ya Isange ili kunusuru maziwa mengi yanayoharibika kwa kukosa soko?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalii hilo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swalii la

Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Maziwa cha Isange kilanza kujengwa na Serikali mnamo mwaka 2012 chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (*Agricultural Sector Development Programme – ASDP – Phase I*). Kupitia programu hiyo shilingi milioni 140 zilitolewa na kutumika kujenga jengo la kiwanda, kuingiza umeme, maji na ununuzi wa tenki la kupoza maziwa (*chilling tank*) lenye uwezo wa lita 2,030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uibuaji wa ujenzi wa Kiwanda cha Maziwa cha Isange ultokana na ukosefu wa soko la maziwa na hivyo kufanya maziwa mengi kuharibika. Hata hivyo, ujenzi wa kiwanda ulikwama baada ya kumalizika kwa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza (*ASDP I*) ambayo ilikuwa ikifadhilli mradi wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ilitangaza fursa ya uwepo wa jengo la Kiwanda cha Maziwa kwa ajili ya wawekezaji ambapo mwekezaji *ASAS DAIRIES LTD* alijitokeza na kuomba kuwekeza katika jengo la Kiwanda cha Maziwa. Mwekezaji baada ya kuingia mkataba na halmashauri ameanza kutumia jengo hilo kama Kituo kikubwa cha kukusanya maziwa yanayonunuliwa kutoka kwa wafugaji kupitia Ushirika wa Wafugaji wa Maziwa wa UTAMBUZI. Kwa sasa mwekezaji anakusanya jumla ya lita 3,600 za maziwa kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji ameahidi kufunga mitambo ya kuchakata maziwa kama kiasi cha maziwa kitaendelea kuongezeka. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wafugaji wa huko Busekelo kutumia fursa hii kuongeza uzalishaji wa maziwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakibete, swalii la nyongeza.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuhusiana na swali hili, hasa hasa ujenzi wa Kiwanda cha Maziwa kule Isange, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wananchi wa Jimbo la Busokelo hasa Kata za Lupata, Kandete, Luteba, Mpombo, Isange, Lwanga, Kabula pamoja na Itete, wanafuga sana ng'ombe wa maziwa wapatao zaidi ya 35,000 na wanazalisha lita zaidi ya milioni 54 kwa mwaka lakini mbegu walizonazo bado ni ng'ombe wale wa zamani. Je, Serikali itawasaidiaje kupata ng'ombe wapya ambapo inaweza kufanyika kitu kinaitwa uhimilishaji kwa ajili ya uzalishaji zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi hawa pamoja na ufugaji wao wanajitahidi sana kukusanya maziwa na kupeleka sehemu ambapo kuna matenki kwa njia ya baiskeli pamoja na pikipiki. Je, Serikali itawasaidiaje kutafuta ama kupata gari la kisasa lenye tenki ili liwasaidie kwa ajili ya kukusanya kwa wakulima na wafugaji ambao wanafuga ng'ombe hawa wa maziwa mpaka sehemu ya viwanda?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali hili, naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mwakibete kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kuhakikisha kwamba wapiga kura wake wa pale Busokelo Rungwe wanafanya kazi ya uzalishaji na kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameniuliza juu ya programu tuliyonayo kama Serikali ya kuhakikisha kwamba tunasaidia

katika kuondoa kosaafu zile za kizamani na kuboresha kosaafu zetu mpya. Wizara yetu katika mpango mkakati wa mwaka 2018/2019, tumejipanga kuhakikisha tunazalisha ndama wa kosaafu hizi za kisasa wasiopungua milioni moja kwa kutumia njia ya uhimilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndama hawa milioni moja watakaozalishwa watatawanywa katika hal mashauri zetu kwa ajili ya kuendeleza kosaafu mpya hizi zenye tija na thamani zaidi kwa uzalishaji wa maziwa na nyama. Moja katika hal mashauri zitakazonufaika na mpango huu ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ni namna gani tunaweza tukawasaidia wazalishaji wa maziwa kule Busokelo. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana wadau binafsi wanaoshirikiana vyema na Serikali na nampongeza pia Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri hiyo anayoifanya kuwashirikisha wadau hawa binafsi. Wadau wetu wa *ASAS DA/RIES* wanafanya kazi nzuri sana ya kuwaunganisha wazalishaji wa maziwa katika eneo hili la Busokelo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba wamepeleka vyombo vya usafiri kama pikipiki kwa ajili ya kukusanya maziwa. Nafahamu pia ya kwamba wadau hawa wanayo malalamiko madogo madogo, sisi kama Wizara kwa kuititia Bodi yetu ya Maziwa tunafahamu malalamiko yao, tayari tunayafanya kazi katika kuleta utengamanisho ili wazalishaji wetu wa endeleo kunufaika. Tunawashawishi sasa *ASAS DIARIES* badala ya kutumia pikipiki zile, waingize magari yenye *cold storage* waende kukusanya maziwa ya wananchi wale ili wananchi waweze kupata faida zaidi ya uzalishaji wao wa maziwa haya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali fupi la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma ni mionganini ya mikoa yenye mifugo mingi sana ikiwemo ng'ombe na kuna nyakati wafugaji wanakosa soko. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhamasisha wadau na wawekezaji mbalimbali ili waweze kujenga Kiwanda cha Maziwa na *collection centre* katika Mkoa wa Dodoma? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wetu ni kuhakikisha kwanza vile viwanda vyetu tulivyonavyo vinafanya kazi ya kuchakata mazao ya mifugo. Hapa Dodoma tunacho kiwanda kikubwa cha *TMC* ambacho hivi karibuni utendaji wake wa kazi haukuwa mzuri sana lakini Wizara tumeingilia kati tunahakikisha kwamba kiwanda chetu hiki kinafanya kazi nzuri ya uchakataji wa mazao ya mifugo kwa maana ya uchinjaji na hatimaye kutengeneza zile nyama kwa ajili hata ya kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake ni kujua namna tunavyoweza kuwavutia wawekezaji wa Kiwanda cha Maziwa hapa Dodoma. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wana Dodoma wote kwamba ombi hili la kuhakikisha tunakuwa na Kiwanda cha Maziwa hapa Dodoma tunalichukua na tutahakikisha kwamba Dodoma na yenye pia inakuwa *centre* nzuri ya kuhakikisha tunatengeneza mazao ya mifungo ikiwemo maziwa na kuyasambaza kote katika nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi. Hilo ndiyo swali letu la mwisho kwa siku ya leo.

Nina matangazo hapa, kwanza ni wageni ambao wapo katika Bunge letu asubuhi hii. Naanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wanne wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana watoto wetu. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambao ni familia yake kutoka Karatu, Mkoani Arusha, wakiongozwa na mke wake Ndugu Ana Mayo. Karibuni sana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Joel Mwaka Makanya ambao ni watumishi wa *Moshi International School* kutoka Mkoani Kilimanjaro. Karibuni. (*Makofi*)

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba, ambaye ni binti yake kutoka Kigoma, Ndugu Tizla Mahushi. Karibu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni mwanachama wa CCM toka Songea Mkoani Ruvuma, Ndugu Arnold Ngonyani. Karibu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko ambaye ni rafiki yake kutoka Kisasa Jijini Dodoma, Ndugu Joyce Mango. Huyu ni fundi wake ambaye anamshonea nguo zake za vitenge, ndio maana mnamuona Mheshimiwa Esther anavyopendeza na vitenge vyake, nami nitaomba urafiki ili nishonewe kama yeye. (*Makofi*)

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Martin Msuha ambao ni marafiki zake kutoka Jiji Dar es Salaam. Karibu. (*Makofi*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Mussa Mbarouk ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Sururu Hashim. Karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Kemilembe Lwota ambaye ni rafiki yake kutoka Jiji la Mwanza, Ndugu Francis Ismail. Karibu sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Allan Joseph Kiula ambaao ni viongozi wa CCM toka Mkalama Mkoani Singida. Karibu sana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Wageni 16 ni wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini ambaao ni Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Maswa. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni watatu ni Mheshimiwa Mwita Waitara, ambaao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Lucy Thomas ambaye ni mke wake. Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waitara. (*Makofi*)

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka ambaao ni Madiwani na wakandarasi kutoka Karagwe, Mkoa wa Kagera. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni wanne ambaao ni Wanakwaya wa Kwaya ya Uinjilisti Usharika wa Kipukwe kutoka Wilaya ya Misenyi Mkoa wa Kagera. (*Makofi*)

Wageni wengine ni walimu 21 waliosoma Chuo cha Ualimu Kasulu, Mkoani Kigoma. (*Makofi*)

Pia tunao wageni hapa wa Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri ambaao ni binamu zake kutoka Dar es Salaam, Nasma Nassoro Suleman na Hawa Hussein Masasi. Karibuni sana binamu zetu katika Bunge letu. (*Makofi*)

Tuna tangazo moja kutoka kwa Naibu Waziri, Wizara ya Mambo ya Ndani Mheshimiwa Masauni ambaye anawatangazia Wabunge wote wanaoishi maeneo ya Kisasa kuwa wanaalikwa kwenye Uzinduzi wa Vituo vya Polisi leo saa 7.00 mchana hapo hapo Kisasa. Mgeni Rasmi atakuwa ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mwongozo wa Spika.

MBUNGE FULANI: Lubeleje. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mwongozo.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nakumbushia tarehe 14 Juni, 2018 niliomba mwongozo kuhusu tangazo la Mheshimiwa Waziri la kuzuia uuzaaji...

MWENYEKITI: Unatumia Kanuni ipi?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Naam?

MWENYEKITI: Kanuni ipi unatumia?

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Kanuni ya 68(7) ya siku hiyo, Waziri alitoa tangazo kwamba...

MWENYEKITI: Yaani Kanuni ya siku hiyo? (*Kicheko*)

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni 68(7) iko wakati wote. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri alitoa tangazo la kutonunua na kuuza damu katika hospitali zetu, nikataka kujua Serikali imejipangaje kutohana na akiba ya damu kwa sababu wagonjwa wengi wanakuwa na mahitaji ya damu na wakati mwingine watu wanalazimika kununua damu kwa sababu damu hakuna. Nilitaka majibu nikaambiwa ningejibiwa Jumatatu iliyoleta mpaka leo sijajibiwa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwongozo wangu ninaoomba leo sasa, Waheshimiwa Mawaziri walituambia tukimaliza Bunge watakuja kutembea kwenye Majimbo yetu, tukaomba ratiba ili tujue kila Waziri anafika lini kwenye Jimbo lako. Kwa hiyo, nawaomba Mawaziri watoe ratiba zao leo hapa ili tujue kila Waziri kwenye Jimbo fulani anakwenda tarehe ngapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mwongozo wangu. (*Makof/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Naona huo mwongozo ni kama kukumbushia tu, Waheshimiwa Mawaziri wameshasikia na *time* yoyote wanaweza kuwapeni ratiba kama siyo leo basi ninyi muwe na uvumilivu tu.

Kuhusu suala lile la mwanzo, limeshapitwa na muda jamani. Toka tarehe 14 wewe unasubiri, utapata majibu maana hukuambiwa utajibowiwa Jumatatu unaweza ukapata majibu wakati wowote.

Waheshimiwa Wabunge, namkaribisha Mheshimiwa Spika ili aweze kuendelea na shughuli za leo.

Hapa Spika (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alkilalia Kiti

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu.

NDG. STEVEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

KAULI ZA MAWAZIRI

SPIKA: Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, karibu sana tafadhali utoe kauli.

**Kauli ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
kuhusu Fursa kwa Wasichana Kujipima uwezo katika
Riadha ili waweze kuiwakilisha nchi katika Mashindano
yajayo ya Kimataifa ya Olimpiki,
All-Africa Games na Mengineyo**

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naomba wakati nawasilisha
kauli hii nifanye marekebisho madogo mawili, matatu ya
kiuandishi na naomba yaingie kwenye *Hansard* kama sehemu
ya kauli.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya pili Wizara ya Habari,
Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la
Ushirikiano wa Kimataifa la *Japan (JICA)* inaandaa
mashindano ya riadha kwa wasichana yatakayofanyika
tarehe 24 - 25 Novemba, 2018, Uwanja wa Taifa Jijini Dar es
Salaam.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la mashindano haya
ambayo kwa mara ya kwanza yalifanyika kwa mafanikio
makubwa tarehe 25 na 26 Novemba, 2017 ni kutoa fursa kwa
vijana wote wa kike nchini wenye vipaji katika riadha
waweze kuonesha uwezo wao kwa kushindanishwa na
wenzao kiwilaya na kimkoa na hatimaye Kitaifa ili wanaofikia
kukaribia viwango Kimataifa tuwalee kiufundi ili
watuwakilishe katika mashindano yajayo ya Kimataifa
yakiwemo *All-Africa Games (2019)* na Olimpiki (*Tokyo, Japan 2020*).

Mheshimiwa Spika, mashindano haya ambayo
yanafadhiliwa kitaifa na *JICA* kwa kushirikiana na Wizara
yamepewa jina la '*Women Pre-Olympics Trials towards the
2020 Tokyo Olympics*' yatahusisha wilaya zote za Tanzania
ambazo zitatoa wanariadha bora watano na kiongozi au
mwalimu mmoja wa michezo kwa kila mkoa. Utaratibu huu
ambao tunautumia kwa mwaka wa pili sasa unasaidia sana
nchi iwe na uchaguzi mpana wa vipaji tulivyonavyo nchini
badala ya kutegemea uteuzi wa wanariadha wetu ufanywe
na asasi chache za michezo Jijini Dar es Salaam. Hivyo, kama

ilivyokuwa mwaka 2017 tutakuwa na jumla ya wanamichezo 186 katika mashindano hayo ambao watakapokuwa Jijini Dar es Salaam mpaka wanaondoka, watahudumiwa na JICA kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, wanariadha watatu wa kike waliofanya vizuri kwenye mashindano ya mwaka 2017 wote wakitokea Mkoani Arusha, wanaungana na wanariadha wenzao watano kwenda Nagai City Japan kushiriki kwenye *Nagai Marathon*. Ni safari ya wiki mbili itakayoanzia Dar es Salaam tarehe 14 Oktoba, 2018. Nagai City ni Jiji ambalo limechagua kuwa mwenyeji wa Timu ya Tanzania kwenye mashindano ya *Olympic yatakayofanyika Japan* mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wote wa Mkoa wa Arusha kwa kutoa wanariadha wote watatu bora wanaotokana na michezo ya mwaka 2017 kwenda Nagai Japan miezi mitatu ijayo.

Mheshimiwa Spika, historia inaonesha miaka ya 60, 70 na 80 tulikuwa na wanariadha wazuri sana wa kike kama akina Mwinga Mwanjala, Nzaeli Kyomo, Restituta Joseph, Rwiza John na kadhalika ambao walililettea Taifa letu sifa na heshima kubwa katika michezo. Vilevile historia inaonesha kuwa Medali ya Kwanza Kimataifa ya riadha ililetwa nchini Tanganyika wakati huo na Mwanariadha Theresia Dismas ambaye alishinda michezo wa kurusha kisahani mwaka 1965 wakati huo ni Tanzania tayari, miaka minne tu baada ya uhuru kwenye mashindano ya *All Africa Games* nchini Congo Brazzaville. Rekodi hii iliyo tukuka ya michezo haikuendelezwa baadaye kutokana na kukosekana kwa msukumo stahili wa michezo ambao sasa tumeurejesha.

Mheshimiwa Spika, ili kampeni hii ya kupata wanariadha bora wa kike nchi ifanikiwe, niruhusu kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote wahakikishe kwamba wilaya zao zinafanya uteuzi wa wasichana bora kwenye

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

riadha ndani ya miezi miwili ijayo yaani Julai na Agosti ili kuipa mikoa muda wa kutosha kufanya uteuzi wa wanariadha watano na kiongozi yaani mwalimu mmoja ambao watasafirishwa hadi Dar es Salaam kabla ya tarehe 24 Novemba, 2018 ,tayari kwa michuano hiyo. Ni matumaini ya Wizara kwamba Waheshimiwa Wabunge watahimiza na kuhakikisha kuwa Wilaya zinatkeleza wajibu wao katika hili na Vyama vya Riadha vya Mikoa na Kamati za Michezo za Mikoa zinashirikiana kwa karibu kufanya uteuzi wa wanariadha bora bila upendeleo au uonevu na kuwasafirisha hadi Dar es Salaam ambako watapokelewa na kupewa chakula na malazi. Tutatoa mrejesho Mkutano ujao wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Tunakushukuru sana kwa kauli hiyo. Katibu.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI- KATIBU WA BUNGE:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kutunga Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (A Bill for an Act to Declare Dodoma City to be the Capital City of the United Republic of Tanzania)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo Kumi na Tatu (13) kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali zipatazo Sita (6) kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika Sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika Sheria hizo (*A Bill for an Act to Amend Certain Written Laws*)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuanzisha Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania kwa lengo la kuinua Kiwango cha Taaluma ya Ualimu na kupata Walimu Mahiri, Kuanzisha Mfumo wa Usajili wa Walimu, Kutoa Leseni za Kufundishia kwa Walimu na Kuweka Vigezo na Viwango pamoja na mambo yanayohusiana na hayo (*A Bill for an Act to Establish The Tanzania Teacher's Professional Board to deal with Professional Competence and Practice, Maintenance of Register of Professional Teacher's and to issue license for Practicing teaching, Maintenance and establishment of Teacher's Professional Standard and Conduct and to provide for the other related matters*)

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kufanya Marekebisho katika Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuondoa upungufu ambao umebainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo (*A Bill for an Act to Amend the Public Private Partnership Act in order to keep the Law updated with challenges observed in its implementation*)

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

SPIKA: Ahsante sana Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona tumesoma kwa mara ya kwanza Miswada mitano ambayo ndiyo tutashughulika nayo kwenye Bunge Ijalo. Katika Miswada

hiyo mitano upo pia Muswada wa Sheria wa kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. (*Makofi*)

Ningependa kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa Muswada huu kuwa mojawapo ya Miswada ambayo inayokuja. Huu ndiyo Muswada ulioahidiwa kwa miaka mingi sana kuliko Muswada mwingine wowote nchi hii lakini ukawa haufiki hapa Dodoma Bungeni. Kwa hiyo, sasa safari hii tunatumaini tutautendea haki ili jambo hili liwe la kisheria. (*Makofi*)

Kwa hiyo, moja kwa moja niseme kwamba Muswada huu wa masuala ya Mji Mkuu wa Dodoma, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ndiyo mtakaoushughulikia tutakaporudi Bunge Ijalo. Kwa hiyo, muanze kupitia mara tu utakapopatikana.

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.2 wa mwaka 2018 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.3 itaenda Kamati ya Katiba na Sheria ya Mheshimiwa Mchengerwa.

Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wenyewe tutapeleka kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ya Mheshimiwa Serukamba. Kwa hiyo, muanze kuijandaa kuupitia Muswada huo na kuutendea haki. (*Makofi*)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, wenyewe utaenda Kamati ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, Kamati ya Bajeti. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, natumaini mmelewa mgawanyo wa kazi kwa maana ya Kamati zitakazopitia Miswada hii. Kamati nydingine nazo tunategemea kupata ratiba zao muda siyo mrefu ili tuweze kupanga ratiba vizuri tunaporudi Bunge Ijalo. Katibu.

NDG. NENELWA WANKANGA - KATIBU MEZANI:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

SPIKA: Taarifa ya Katibu wa Bunge.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Kwa heshima na taadhima, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kututolea Hoja ya Kuahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. (*Makofii*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema kwa kutufikisha siku hii ya leo tukiwa na afya njema ambapo tunahitimisha Mkutano huu wa Kumi na Moja ulioanza siku ya Jumanne tarehe 3 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru wewe mwenyewe binafsi, lakini pia namshukuru Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki kikamilifu katika Mkutano huu tangu tulipoanza vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge na baadaye Mkutano wa Bunge. Katika Mkutano huu tumeweza kutekeleza kikamilifu wajibu wetu wa Kikatiba kwa kujadili na kuitisha bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mtakubaliana nami kuwa bajeti hii inatoa mwelekeo mzuri wa utekelezaji wa ahadi mbalimbali za Serikali kwa wananchi kama ilivyoainishwa kuititia llani ya Uchaguzi ya

Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020, pamoja na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipokuwa anafungua rasmi Bunge la Kumi na Moja tarehe 20 Novemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26 Mei, 2018, Bunge lako Tukufu lilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Kasuku Bilago aliyekuwa Mbunge wa Buyungu, Kigoma. Nitumie nafasi hii kukupa pole wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, mke wa marehemu, watoto, familia kwa ujumla na wananchi wote wa Buyungu kwa kumpoteza Mwakilishi wao huyu aliyekuwa na mchango mzuri kwenye Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani Mbunge wa Korogwe Vijijini na kwa Mheshimiwa Angeline Sylvester Mabula, Mbunge wa Ilemela Mkoani Mwanza kwa kufiwa na wenza wao.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia nitoe salamu zangu za pole na kuwatakitia afya njema na uponyaji wa haraka Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote ambao hawako nasi hapa Dodoma kutokana na sababu mbalimbali za kiafya. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu wapone haraka na kuendelea kulitumikia Taifa letu pamoja na wapiga kura wao. Wabunge hao ni Mheshimiwa Haji Ameir Haji, Mbunge wa Makunduchi; Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mbunge wa Butiama; Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki; Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge Korogwe Vijijini; na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Spika, vilevile tarehe 14 Juni, 2018 tulipokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa taarifa ya vifo ya vijana wetu 10 wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Afisa mmoja wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Dereva na Kondakta wa Basi walilokuwa wakisafiria kuelekea Itende, Mkoani

Mbeya kwa ajili ya mafunzo ya vitendo. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao na wengine kupata ulemavu katika matukio mbalimbali ikiwemo ajali iliyohusisha basi dogo la abiria na lori la mchanga eneo la Dundani, Wilayani Mkuranga, Mkoani Pwani na kuua watu zaidi ya 14. Pia juzi tumpata taarifa ya gari dogo lililoua abiria zaidi ya watano Mkoani Mtwara. Tuendelee kuwaombea marehemu wote Mungu aweke roho zao mahali pema peponi na tuwaombee majeruhi wote, Mungu awape nafuu na waweze kupona haraka.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Endrew Chenge (Mtemi), Mbunge wa Baridi; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala; na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa tena kumsaidia Mheshimiwa Spika, kuliongoza Bunge kwa Awamu hii. Mtakubaliana nami kwamba Wenyeviti hawa wameendelea kufanya kazi ya kuongoza vikao vyetu vizuri, kwa busara na umakini mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza na kuwashukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha kazi zote zillizopangwa kwenye mkutano huu kwa ufanisi mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika (*PAP*) na Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, Mbunge wa Handeni Vijijini kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Vijana wa Bunge la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, niwapongeze sana Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba na

Mheshimiwa Asha Abdullah Jumaa kwa jina maarufu 'Mshua', Mbunge wa Viti Maalum kwa ushirikiano wao mkubwa uliochangia ushindi wa Mheshimiwa Stephen Julius Masele. Ushindi wake umelipa heshima kubwa Bunge letu na Taifa kwa ujumla. Pia Serikali itaendelea kushirikiana na Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika pamoja na Rais wa Umoja wa Vijana wa Afrika ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa majibu mazuri waliyoyatoa wakati wa kujibu maswali mengi ya msingi na ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge pamoja na kujibu hoja za Kamati za Kudumu za Bunge zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kipindi chote cha Bunge hili. Serikali inaahidi kuendelea kuzingatia maoni na ushauri ultiotolewa na Waheshimiwa Wabunge na tutaufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Serikali na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha katika kufanikisha shughuli zote za Bunge la Bajeti. Mwisho, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake wote kwa kuandaa Miswada ya Sheria na Maazimio yaliyowasilishwa kwenye Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, tunapohitimisha mkutano huu, tumeweza pia kukamilisha mjadala wa Miswada miili, kuititia Maazimo ya Bunge mawili na kupokea Kauli sita za Serikali. Aidha, Serikali ilipokea maswali ya msingi, ya nyongeza na ya papo kwa papo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, jumla ya maswali 530 ya msingi na mengine 1,705 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge. Maswali hayo yalijibowi na Serikali kuititia kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri na kipindi cha maswali cha papo kwa papo kwa Waziri Mkuu. Katika kipindi hiki, Ofisi ya Bunge iliendesha

semina mbalimbali kwa Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi na kuwapa uelewa mpana wa masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia Bunge lako Tukufu limejadili na kupitisha bajeti za Wizara zote 21 na bajeti nzima ya Serikali Kuu. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha na Matumizi wa mwaka 2018 (*The Appropriation Bill, 2018*) na Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2018 (*The Finance Bill, 2018*) ilijadiliwa na kupitishwa kwa hatua zake zote.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Mkutano huu wa Bunge, Bunge lako liliridhia Maazimio mawili ambapo la kwanza ni Azimio la Bunge la Kuridhia Makubaliano ya Paris chini ya Mkatuba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadilliko ya Tabianchi (*The Paris Agreement Under the United Nations Framework Convention on Climate Change*). La pili ni Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuendeleza Mji wa Dodoma na kuupa hadhi ya Jiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaungana na Bunge lako Tukufu kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi huu muhimu ambaao naamini utasaidia kuendeleza kwa kasi Jiji letu la Dodoma. Aidha, katika kuhakikisha Jiji la Dodoma linaepukana na adha ya kuwa na msongamano wa magari, Serikali ina mpango wa ujenzi wa barabara ya pete (*outer ring road*). Barabara hiyo yenye urefu wa kilometra 104 itahusisha maeneo ya Mtumba, Veyula, Nala na Matungulu. Kukamilika kwa barabara hiyo ambayo ipo katika hatua ya usanifu, kutasaidia Jiji la Dodoma kukabiliana na changamoto za msongamano barabarani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu, Serikali ilitoa Kauli mbalimbali za Serikali, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

- (i) Kauli ya Serikali kuhusu Watumishi Walioondolewa kwenye Mfumo wa Malipo ya Mshahara kwa Kukosa Sifa ya Cheti cha Kufaulu Mtihani wa Elimu ya Kidato cha Nne;
- (ii) Kauli ya Serikali kuhusu Matumizi ya Shilingi triliungi 1.51;
- (iii) Kauli ya Serikali kuhusu Upungufu wa Mafuta ya Kula;
- (iv) Kauli ya Serikali kuhusu Kuibuka kwa Ugonjwa Mpya kwenye Zao la Korosho;
- (v) Kauli ya Serikali kuhusu Katazo la Serikali la Kusafirisha *Activated Carbon* kutoka Mkoa Mmoja kwenda Mwingine;
- (vi) Kauli ya Serikali kuhusu Maafisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Kuingia katika Mgahawa wa Bunge Kufanya Ukaguzi wa Samaki Waliovuliwa Kimakosa;
- (vii) Kauli ya Serikali kuhusu Fursa ya Wasichana Kujipima Uwezo katika Riadha ili Waweze Kuiwakilisha nchi kwenye Mashindano Yajayo ya Kimataifa ya *Olympic* ya *All-Africa Games* na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Serikali wa mwaka 2018/2019. Mkutano huu tunaohitimisha leo, ulikuwa mahsus kwa ajili ya kujadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango mingi na mizuri mliyoitoa wakati wa mjadala wa hoja kuhusu Mpango wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuhitimisha mijadala ya bajeti za Wizara, ilionekana dhahiri kwamba muda haukutosha kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kutokana na hali hiyo, kama walivyoahidi Waheshimiwa

Mawaziri wakati wa majumuisho ya hotuba za Wizara zao, Serikali itaendelea kutoa majibu na maelezo ya ufanuzi kwa maandishi kwa zile hoja ambazo hazikupata nafasi ya kujibiwa kwa sababu ya ufinyu wa muda. Nami napenda nitumie muda huu kutoa maelezo machache ya ufanuzi kwa baadhi ya maeneo machache nikiamini mengi yalikuwa yameshajibiwa na Wizara husika wakati wa mijadala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi trillioni 32.48 na kati ya fedha hizo, shilingi trillioni 20.47 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 63 ya bajeti ya shilingi trillioni 12.01 na asilimia 37 ya bajeti yote zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kuitisha bajeti hii nzuri ya Serikali yenye dhamira ya kuendelea kujenga uchumi wa viwanda utakaochochaea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Nawasihi sana Watanzania wote pamoja na wadau wa maendeleo tushirikiane kwa pamoja katika utekelezaji wa bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itasimamia ipasavyo utekelezaji wa bajeti sambamba na kuongeza uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya fedha zote zilizolekezwa katika vipaumbele mbalimbali kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali kadhalika, Serikali itaimarisha ukaguzi katika ngazi zote na ufuatiliaji wa karibu wa miradi ya maendeleo na kufanya tathmini za mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba miradi na kazi zitakazofanyika zinawiana na thamani ya fedha za umma zinazotolewa na Serikali (*value for money*). Katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali itashirikiana na sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi wote kwa ujumla ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba malengo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi yanazingatia bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imetoa maelekezo kwa

Watendaji wa Serikali katika ngazi zote kuwajibika ipasavyo katika ukusanyaji wa mapato na kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha na rasilimali za Taifa. Viongozi na Watendaji wote wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma katika eneo la ukusanyaji wa mapato. Vilevile taasisi zote za Serikali zinasisitizwa kutumia mifumo ya kielektroniki kukusanya mapato na wafanyabiashara wote wanahimizwa kutumia mashine za *EFD* na kulipa kodi kwa hiari yao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo na mifugo. Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II). Moja ya maeneo ambayo yalikuwa na hoja nyingi katika mjadala wa Bunge la Bajeti ni suala la kilimo hususan uendelezaji wa mazao makuu ya biashara na chakula na uwekezaji katika kilimo. Hata hivyo, napenda kujulisha Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 4 Juni, 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alizindua Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini (*Agricultural Sector Development Program Phase II*). Lengo la programu hii ni kuongeza tija na uzalishaji katika mnyororo wote wa thamani (*value chain*) ili kuvipatia malighafi viwanda vitakavyoanzishwa na kupata ziada ya chakula na kuuza katika masoko ya nje ya nchi kwa lengo la kupata faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, programu hiyo inaweka mkazo katika maeneo makuu manne kama ifuatavyo:-

(i) Usimamizi endelevu wa matumizi ya ardhi na maji katika kilimo;

(ii) Kuongeza tija na faida katika kilimo, mifugo na uvuvi;

(iii) Kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuongeza thamani ya mazao; na

(iv) Kuwajenjea uwezo wadau wa sekta katika uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi na sekta nyingine zote watumie fursa mbalimbali zinazopatikana katika programu hii ili kutimiza ndoto ya nchi yetu kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Aidha, naagiza taasisi zote zinazohusika na utekelezaji wa *ASDP* // ziimarishe usimamizi na ufuatiliaji ili utekelezaji wa programu hii uwe wa mafanikio makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo imeweka kipaumbele kuendeleza mazao ya kilimo yakiwemo mazao makuu matano ya biashara ambayo ni pamba, tumbaku, korosho, kahawa na chai kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Serikali itaimarisha mifumo ya usimamizi wa mazao hayo katika ngazi zote kuanzia kijijini hadi Taifa. Maafisa Ugani, Maafisa Kilimo na Maafisa Ushirika wawe tayari na wameshapewa maelekezo mahsusni katika kutekeleza jukumu hilo. Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kufufua na kuimarisha ushirika ili uwe mhimili wa kusimamia masoko na upatikanaji wa bei nzuri kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mazao makuu ya kimkakati, Serikali imeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa mazao mengine yanapewa kipaumbele kwa kuwapa Maafisa Kilimo malengo ya kusimamia kwa ukamilifu maandalizi na upatikanaji wa pembejeo na masoko yake. Mazao hayo ni pamoja na ufuta, alizeti, michikichi, mkonge, zabibu, pareto, ngano na mengineyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mazao haya, tumeamua kuyauza kwa mfumo wa Stakabadhi Ghalani na mfumo huu umekuwa na mafanikio katika maeneo mengi nchini. Hii ni kwa sababu wakulima wadogo na wa kati wanakuwa kwenye ushirika na hivyo kuwa na nguvu ya pamoja ya soko ya kuwapatia wakulima bei nzuri ya mazao yao. Mathalan kwa kutumia mfumo huo, mwezi huu bei ya ufuta

imeongezeka kutoka Sh.1,500 ya mwaka 2017 hadi Sh.2,840 kwa kilo na kuua mfumo usio rasmi wa uuzaji wa zao hilo ujulikanao kama Chomachoma ambao ulimpunja mkulima kwa ujazo na bei. Aidha, mfumo huu unasaidia kuzuia upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi dhaifu. Pia unasaidia kuhifadhi mazao ili kusubiri kuuza wakati muafaka na kuyaongezea mazao thamani kabla ya kuyauza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua kadhaa kuhakikisha kuwa mfumo huu unatekelezwa kikamilifu na kuleta tija kwa wakulima. Hatua hizo ni pamoja na ushirikishwaji muhimu wa wadau, kuimarisha ushirika, kuweka miundombinu ya masoko na kuboresha muundo wa taasisi na vitendea kazi vya Bodi ya Stakabadhi za Ghala. Natoa wito kwa Watendaji Serikalini kuhakikisha kuwa mazao mengi zaidi yanaingizwa katika Stakabadhi za Ghala ili kuwe na tija kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie soko la muhogo lililopo nchini China. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imetoa fursa kipekee kwa Tanzania ya kufungua soko la muhogo mkavu kutoka huku kwetu Tanzania. Ili kuwezesha wakulima na wafanyabiashara wa Tanzania kunufaika na fursa hiyo, Mei, 2018 ulisainiwa Mkataba katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuruhusu bidhaa za muhogo mkavu kutoka Tanzania kuingia katika soko la China. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, mwezi huu wa Juni, 2018, jumla ya tani 74 za muhogo mkavu kutoka Tanzania zimeingia nchini China kupitia Bandari ya Qingdao iliyopo Jimbo la Shandong. Tukio hili la kihistoria linafungua ukurasa mpya wa zao la muhogo kuwa mionganoni mwa mazao ya biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiasi cha muhogo tunachomudu kuingiza katika soko la China bado ni kidogo ukilinganisha na mahitaji ambayo yanazidi tani 150,000 kwa mwaka. Nitoe wito kwa Watanzania wahangamkie fursa ya kilimo cha

muhogo ambacho kimeonyesha kuwa na tija kubwa. Hali kadhalika, nitoe rai kwa mamlaka zetu hususan Vituo vyatya Utafiti wa Kilimo kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora na mbinu za kisasa ili kuweza kuongeza uzalishaji na kuza muhogo nchini China kwa faida kubwa sambamba na kukidhi mahitaji ya soko hilo. Kutokana na zao la muhogo kuonekana kuwa na matumizi mengi zaidi ya chakula, Serikali inaendelea kuvutia uwekezaji wa viwanda vyatya kuchakata muhogo na kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sekta ya ardhi. Serikali imeendelea kukabiliana na changamoto ya migogoro ya matumizi ya ardhi mionganoni mwa watumiaji kwa kuunda timu za kisekta ikijumuisha watendaji wa sekta mbalimbali zinazohusika kwa njia moja au nyngine kwenye masuala ya migogoro ya ardhi. Sambamba na hilo, Serikali imeandaa mipango ya matumizi ya ardhi, kupima mipaka ya vijiji, kutunga na kurekebisha sera, sheria na kuandaa programu mbalimbali na kuboresha matumizi ya utawala wa ardhi. Kadhalika, Serikali imeandaa programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Ni matumaini yangu kwamba programu hii ikitekelezwa ardhi itatoa mchangano mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii na pia kudhibiti migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali itaendelea kutatua migogoro inayojitokeza na pia kutoa elimu kwa umma namna bora ya matumizi ya ardhi kwa watumiaji wote wa ardhi ili waweze kuzingatia mipango ya matumizi ya ardhi inayoandalawa katika vijiji na ngazi nyngine. Katika juhudini za kudhibiti migogoro kwenye maeneo mbalimbali ya utawala, jumla ya vijiji 11,256 katil ya vijiji 12,545 vilivyopo hapa nchini vimepimwa. Hii ni sawa na asilimia 90 ya vijiji vyote vilivyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kupima mipaka ya vijiji vyote vilivyopo na kuvipatia Vyeti vyatya Kijiji kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo. Hatua hii itasaidia kwa kiwango kikubwa kutatua migogoro ya mipaka katil ya vijiji. Ili kuhakikisha kwamba kasi ya upimaji nchini inaongezeka,

Serikali itaendelea kutumia makampuni binafsi ya upimaji kwa upangaji wa makazi kwa vibali maalum.

Mheshimiwa Spika, sekta ya utalii. Kutokana na jitihada za Serikali katika kulinda rasilimali za nchi na ushirikiano kutoka kwa wananchi, idadi ya wanyama porini imeongezeka hivyo kulifanya Taifa kuwa nchi yenye wanyama wengi Barani Afrika. Ili kuitumia vyema fursa ya kuwa na vivutio vingi ikiwemo wanyamapori wengi na kuleta tija kwa nchi, Serikali imeendelea kuandaa Utambulisho wa Tanzania Kimataifa (*Destination Branding*). Lengo la utambulisho huo ni kuitambulisha Tanzania kama kituo mahsus cha utalii duniani cha kuvutia wageni wa Kimataifa kuitembelea Tanzania, kuongeza wigo wa kutangaza vivutio na kufanya vivutio vya utalii Tanzania vifahamike duniani kote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali inakamilisha mchakato wa kuanzisha *channel* maalum katika Televisheni ya Taifa (*TBC1*) kwa ajili ya kutangaza utalii. Pia Serikali inaendelea na mpango wa kuanzisha chombo kitakachosimamia fukwe za bahari, mito na maziwa chenye lengo la kuhakikisha kwamba fukwe hizi zinatumika pia kitalii. Lengo la hatua hiyo ni kuimarisha utalii wa fukwe za bara na visiwani kwa kujenga mahoteli, maeneo ya mapumziko na maeneo ya michezo mbalimbali ya majini. (*Makof*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tumsikilize Mheshimiwa Waziri Mkuu jamani. (*Makof*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, pia maandalizi ya kuanzisha studio ya kutangaza utalii kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanaendelea vizuri. Studio hiyo itawezesha kutambua, kufuatilia na kuwasiliana moja kwa moja na watu wanaofuatilia vivutio vya Tanzania kwa njia ya TEHAMA. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la hifadhi za mazingira. Misitu yetu inaendelea kukatwa hovyo kwa sababu mbalimbali ikiwemo matumizi ya nishati ya mkaa na kuni. Ili kuendeleza matumizi ya nishati mbadala

nchini, Serikali itashirikiana na sekte binafsi kuweka utaratibu mahsuswa wa kuwawezesha na kuratibu wajasili amali wanaojishughulisha na nishati mbadala ili kuwe na uzalishaji wa kutosha wa nishati na iweze kusambazwa kote nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha na kukamilisha Mkakati wa Tungamotaka (*National Biomass Energy Strategy*) na kusambaza kwa wadau nchini ili kuratibu vyema upatikanaji wa utumiaji wa nishati hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa umeme wa kutosha wa uhakika na usiotegemea chanzo kimoja umeendelea kuwa kipaumbele kwa Serikali ya Awamu ya Tano. Serikali imeendelea kuchukua hatua za makusudi kuzalisha umeme utakaoiwezesha nchi kufikia hatua ya uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Kwa kuzingatia hilo, Serikali inaendelea kutoa kipaumbele katika matumizi ya vyanzo mbalimbali vya nishati ya umeme ikiwemo maji, gesi, makaa ya mawe, jotoardhi, jua, upepo na tungamotaka. Mathalan kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa maji katika Mto Rufiji wa *Megawatt* 2,100. Pia iko katika hatua ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa umeme wa jua Mkoani Shinyanga wa *Megawatt* 150 na mradi wa umeme wa upepo Mkoani Singida wa *Megawatt* 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wengi walishauri Serikali iharakishe utekelezaji wa mpango wa usambazaji wa umeme vijijini ili maeneo mengi katika Majimbo yao ambayo hayana umeme yaweze kufikiwa na huduma hiyo ya umeme. Aidha, wapo ambaao walitaka fedha za *REA* zitolewe kwa wakati na kama ilivyoainishwa na Bunge. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya umeme kwa Awamu ya *Tatu huko Vijijini*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (*Liquified Natural Gas*). Kufuatia ugunduzi wa kiwango kikubwa cha gesi asilia, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) inashirikiana na wawekezaji ambaao ni makampuni ya Kimataifa ya mafuta

kuendeleza rasilimali hiyo na kujenga mradi mkubwa wa kuchakata na kusindika gesi asilia (*Liquified Natural Gas - LNG*) kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020. Mradi huo ambao unatumia gesi asilia iliyogundiwa kwenye kina kirefu cha bahari una lengo la kuiwezesha Tanzania kuvuna na kuuza rasilimali ya gesi katika Soko la Dunia sambamba na kukidhi mahitaji ya soko la ndani yanayojumuisha matumizi ya viwandani na majumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mradi huo mkubwa wa aina yake na wenye maslahi mapana kwa Taifa letu unatekelezwa kama ulivyopangwa. Aidha, Mradi wa *LNG* unaokadiriwa kugharimu takribani Dola za Marekani bilioni 30 na kuchukua eneo lenye ukubwa wa hekta 2,071.7 pamoja na mambo mengine, una faida zifuatazo:-

- (i) Kuongeza mapato ya Serikali kuitia mauzo ya gesi katika soko la ndani na nje;
- (ii) Upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa ajili ya viwanda na matumizi ya nyumbani;
- (iii) Kuwa chanzo cha malighafi za viwanda kwa ajili ya kuzalisha mbolea, plastiki na kemikali za petroli (*petrol chemical*);
- (iv) Kuwa chanzo cha ajira ambapo wakati wa ujenzi wake mradi huo utaa jiri takribani watu 10,000 na wengine wapatao 3,000 wakati wa uendeshaji; (*Makofii*)
- (v) Kutasaidia ukuaji wa uchumi wa Miji ya Lindi na Mtwara utakaokwenda sambamba na kupanuliwa kwa bandari na uwanja wa ndege; na
- (vi) Kuibua fursa za biashara kwa Watanzania pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kuhusu usimamizi wa miradi ya namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema tukatambua kuwa mradi huu una maslahi makubwa kwa Taifa. Hivyo, Serikali inachukua tahadhari kubwa kwenye majadiliano yanayoendelea baina ya Timu ya Majadiliano ya Serikali (*GNT*) na Makampuni ya Kimataifa ya Mafuta (*IOCs*). Serikali inaendelea na majadiliano na makampuni hayo ya mafuta ili mradi huo uanze kutekelezwa mapema iwezekanavyo kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, msaada wa kisheria. Serikali imeanza utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa kuteua wasaidizi na watoa huduma ya msaada wa kisheria katika ngazi za Mikoa, Majiji, Wilaya na Halmashauri zote nchini. Lengo la Serikali ni kusogeza huduma ya msaada wa kisheria karibu na wananchi. Hivi sasa Wasajili Wasaidizi wanaendelea kupatiwa mafunzo elekezi ya namna ya kuratibu, kusimamia, kutambua na kusajili taasisi mbalimbali zinazotoa na zitakazotaka kutoa huduma hiyo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwasihii Waheshimiwa Wabunge mtakaporudi Majimboni mkawahamasishe wananchi waitumie fursa hii kupata haki zao vizuri. Vilevile ninawaasa wale wote ambao wamepewa dhamana ya kusimamia zoezi hili la kutoa huduma hii wafanye kazi kwa weledi na maadili ili huduma hii iwe endelevu na imsaidie mwananchi wa kawaida kuweza kupata haki yake.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuimarisha mfumo wa utoaji haki nchini, Serikali ilianzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kurekebisha muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nia ya Serikali ni kuimarisha huduma za mashtaka, usimamizi na ufuatilaji wa mashauri ya madai ndani na nje ya nchi ambayo Serikali ina maslahi; kuimarisha pia uwezo wa Wanansheria wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai, lakini pia kuimarisha usimamizi na masuala ya mikataba na kuimarisha uandishi na urekebu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ofisi hizi tatu katika muundo wake mpya zitaanza kazi rasmi Julai, 2018. Nichukue pia fursa hii kuwataka watumishi wote watakaokuwa kwenye ofisi hizi wafanye kazi kwa weledi, uadilifu na umakini katika kutoa huduma ambazo wanapewa dhamana nazo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya. Katika mwaka 2018/2019, Serikali imedhamiria kupunguza vifo vya akina mama na watoto vitakavyotokana na uzazi. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, inaendelea kufanya ukarabati na ujenzi wa majengo ya upasuaji, maabara, wodi za wazazi, nyumba za watumishi na wodi za watoto. Hatua hii itawezesha upatikanaji wa huduma kamili za uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, eneo litakalopewa kipaumbele ni kuimarisha upatikanaji wa vifaa na watumishi katika vituo 208 vinavyoendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha upatikanaji wa damu ikiwa ni pamoja na mikakati ya kupunguza vifo ikiwemo vitokanavyo na uzazi. Kwa mwaka 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.3 ili kujenga vituo vya kuhifadhia damu (*satellite blood banks*) kwenye mikoa 12 na Mikoa hiyo ni Manyara, Katavi, Rukwa, Ruvuma, Njombe, Tanga, Arusha, Pwani, Singida, Songwe, Geita na Simiyu. Lengo la mpango huo ni kuboresha upatikanaji wa damu hususan kwa akina mama wanaopoteza damu nydingi wakati wa kujifungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwasihii watumishi wa afya waongeze juhudii katika kuwahamasisha wananchi kujitolea damu. Niwaombe wananchi wawe na utamaduni wa kuchangia damu ili kuwezesha upatikanaji wa damu na iweze kuhifadhiwa kwenye benki zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa huduma za kibingwa. Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha huduma za kibingwa nchini. Moja ya hatua zinazochukuliwa ni kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Taasisi za Saratani *Ocean Road* ambapo shilingi bilioni 14

zimetengwa kwa ajili ya kuanzisha huduma ya kuchunguza mwili bila upasuaji. Kuanza kwa huduma hiyo, kutapunguza asilimia 80 ya wagonjwa wa saratani waliokuwa wanapelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kipimo hiki na kuokoa takribani shilingi bilioni 5 kwa mwaka zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya kulipia wagonjwa kwenda nje ya nchi kwa ajili ya kipimo hiki.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itasogeza huduma za tiba ya saratani katika ngazi ya Hospitali za Kanda ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Bugando, Mwanza; Hospitali ya Kanda ya Kaskazini, *KCMC*; na Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pale Jijini Mbeya. Vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali itaimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na majengo, vifaa tiba na Madaktari Bingwa. Jumla ya shilingi bilioni 40 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha hospitali hizo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya elimu. Serikali inatambua kutokuwepo kwa miundombinu ya kutosha katika shule za msingi na sekondari. Hali hiyo imechangiwa na ongezeko la uandikishaji wanafunzi wa Elimu ya Awali, Darasa la Kwanza, Kidato cha Kwanza na wale wanaojiunga na Kidato cha Tano kila mwaka ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu Msingi Bila Malipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (*Education Performance for Results*)imeendelea kuimarisha miundombinu muhimu kwenye shule mbalimbali zenye uhitaji mkubwa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali itatumia shilingi bilioni 155.58 kwa ajili ya ukarabati wa shule zote kongwe 25, ununuzi wa vifaa vya maabara, ujenzi wa mabwalo 85, vyumba vya madarasa 2,000 na motisha kwa Halmashauri kutohana na ufanisi katika utekelezaji wa vigezo vya *EPforR*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo, Serikali inaendelea kuajiri walimu wapya. Kwa sasa Serikali inatarajia kuajiri walimu 4,785 wa shule za msingi zenyenye uhitaji mkubwa. Aidha, tayari Serikali imetangaza nafasi za ajira kwa walimu 2,000 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lughu (*Literature in English*) ambao watapangwa kwenye shule za sekondari zenyenye uhitaji mkubwa. Kadhalika, Serikali pia imetangaza nafasi za ajira kwa Mafundi Sanifu Maabara 160 ambao pia watapangwa kwenye shule zenyenye uhaba wa wataalam hao.

Mheshimiwa Spika, sekta ya maji. Wakati wa mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kulikuwa na hoja kuhusu hali isiyoridhisha ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini. Changamoto nyingine iliyozungumzwa ni udhaifu kwenye usimamizi wa miradi ya maji. Maeneo mengi nchini yameendelea kukabiliwa na uhaba wa maji kutokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni pamoja na uharibifu wa vyanzo vya maji, ukataji holela wa miti na uchomaji misitu, ongezeko la watu na mifugo, athari za mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya maji yasiyozingatia tija na ufanisi. Aidha, tatizo la maji pia limechangiwa na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na jamii zinazowiana na uwekezaji katika miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa miradi ya maji inatekelezwa ipasavyo, Serikali imeamua kufanya yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha miradi inayotekelizwa inakuwa bora, yenye kuwiana na thamani halisi ya fedha pamoja na kukamilishwa kwa wakati kama ilivyo katika mikataba. Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa watendaji wote watakaobainika kutotekeliza majukumu yao ipasavyo.

(ii) Kuunda Kamati Maalum itakayochunguza miradi yote ya maji vijijini ili kujiridhisha na utekelezaji wake. Kamati hiyo itatarajiwa kuwasilisha maoni na ushauri utakaowezesha Serikali kuona namna bora ya kusimamia miradi ya usambazaji maji vijijini na mijini. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla

kuipa Kamati ushirikiano wa kutosha ili ikamilishe majukumu yake kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utawala bora na masuala ya wafanyakazi. Utumishi wa umma wenye ufanisi ni nyenzo muhimu ya kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Kwa kutambua hilo, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza ghamama za uendeshaji na urasimu katika utoaji wa huduma, kurejesha nidhamu, uadilifu, uwajibikaji katika utumishi wa umma pamoja na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo, tarehe 23 Juni, 2018, Serikali ilizindua mifumo tisa ya TEHAMA inayohusu utoaji huduma Serikalini. Mifumo hiyo ni Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo, Mfumo wa Taarifa ya Kitabibu, Mfumo wa Taarifa za Ununuizi, Mfumo wa Kumbukumbu za Kielektroniki na Mfumo wa Ofisi Mtandao. Mingine ni Mfumo wa Ankara Pepe na Ulipaji wa Serikali, Mfumo wa Utoaji Huduma za Kiserikali kupitia Simu za Mkononi, Mfumo wa Baruapepe wa Serikali na Mfumo wa Vibali vya Kusafiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mifumo hiyo itahakikisha kuwa huduma zinazotolewa na taasisi za umma zinaboreshw sambamba na kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za Serikali za kila siku. Hivyo, Serikali itaendelea kubuni na kutumia mifumo ya TEHAMA na teknolojia nyingine rahisi na salama kwa lengo la kuwapatia wananchi, hususan wa vijijini, huduma bora na kwa wakati. Viongozi na watendaji wa Serikali hakikisheni kuwa mifumo hiyo haitumiki kukwamisha shughuli za Serikali au mipango ya utoaji huduma kwa wananchi. Aidha, wale wote watakaobainika kuhujumu mifumo hii wachukuliwe hatua za kinidhamu huko huko kwenye maeneo yao ya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kufuatia zoezi la uhakiki wa vyeti vya watumishi wa umma, Serikali ilipokea malalamiko kutoka

kwa watumishi, Vyama vya Wafanyakazi pamoja na Waheshimiwa Wabunge. Hata hivyo, Serikali ilitoa maelekezo kwa waajiri wote nchini kuwarejesha kazini na kuwalipa mishahara stahiki watumishi wote waliokuwa na ajira za kudumu au za mikataba kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa au ajira za muda (*employment on temporary terms*) ambao walikuwa kazini kabla ya tarehe 20 Mei, 2004, pamoja na watumishi wa umma 1,370 waliolezewa masharti ya sifa za muundo. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuboresha huduma kwa wananchi kwa manufaa na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa vijana, wanawake na wale mavu. Serikali itaendelea kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili waweze kupatiwa mikopo yenye masharti nafuu ikilinganishwa na taasisi nyingine za fedha. Sambamba na hilo, naielekeza mikoa na mamlaka ya Serikali za Mitaa zihakikishe zinatenga kiwango hicho cha asilimia 10 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na zisaidie uundaji wa *SACCOS* shirikishi za makundi haya ili wote waweze kunufaika na fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nielekeze mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazijakamilisha uundaji wa Kamati za Kuhudumia Watu Wenye Ulemavu, zihakikishe Kamati hizo zinaundwa ikiwa ni pamoja na kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Napenda kusitiza kuwa yatengwe maeneo mahsus kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa urahisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huduma za hifadhi ya jamii. Katika kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii hapa nchini, mapema mwaka huu Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria Na. 2 ya mwaka 2018 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na sheria hiyo imeunganisha Mifuko ya Pensheni ya *PPF*, *PSPF*, *GEPF* na *LAPF* na kuunda Mfuko mpya wa kuhudumia watumishi wa Umma ujulikanao kama *PSSSF*. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NNSF*) umefanyiwa marekebisho ili uweze kuhudumia sekta binafsi na isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taratibu za kuunganisha mifuko hii zimekamilika na mifuko hiyo itaanza kutoa huduma hizi karibuni. Hatua hii itaboresha huduma za hifadhi ya jamii katika ngazi zote ili hatimaye wananchi wasilazimike kufuata huduma hizo makao makuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, utamaduni na michezo. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo litalenga kutangaza na kuuza kazi za kiutamaduni na ubunifu, filamu, utalii na masuala mbalimbali ya kihistoria. Tamasha hili linatarajiwu kuleta wajasiriamali na wadau mbalimbali wa sekta za utamaduni, sanaa na michezo na ubunifu zaidi ya 1,200 kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika tamasha hilo tunatarajia kuwashirikisha zaidi wajasiriamali wa kazi za kiutamaduni, sanaa na ubunifu takribani 20,000 kutoka mikoa mbalimbali nchini. Hivyo, natoa wito kwa wadau mbalimbali wajitokeze kufanikisha tamasha hilo lenye manufaa makubwa kwa Taifa letu ikiwemo kuimarisha masoko ya bidhaa za viwanda na kazi za kiutamaduni, sanaa na ubunifu pamoja na kuitangaza Tanzania na fursa zake nyingi za kipekee zilizopo. Aidha, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wajasiriamali wetu kwenye maeneo yetu kwa kuandaa kazi za utamaduni, sanaa na ubunifu na filamu katika maeneo yao ili waweze kujitokeza kwa wingi kutumia fursa hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2018/2019, Tanzania pia itakuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu wa vijana chini ya umri wa miaka 17 (*AFCON Under 17*). Hii ni fursa nyingine ya kipekee ambayo inakuja nchini kwetu ya kutangaza Taifa letu katika nyanja za Kimataifa. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na maandalizi stahiki ambayo yatahusisha pia ukarabati wa miundombinu ya viwanja vitakavyotumika katika mashindano hayo. Natoa wito kwa wananchi watumie vizuri uwepo wa mashindano hayo kujiongezea kipato, hususan kupitia biashara ya bidhaa na huduma kwa wageni. Pia tuiunge mkono timu yetu

itakayoshiriki mashindano hayo iweze kupata mafanikio.
(Makofî)

Mheshimiwa Spika, kampeni dhidi ya UKIMWI na VVU. Itakumbukwa kuwa Desemba Mosi, 2017 katika maadhisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua matokeo ya awali ya utafiti wa nne kuhusu viashiria vya VVU na UKIMWI. Utafiti huo uliofanyika katika ngazi ya kaya kuanzia Oktoba, 2016 hadi Agosti, 2017 ulionesha kuwa hamasa ya upimaji wa VVU ni ya kiwango cha chini hususan kwa wanaume.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, tarehe 19 Juni, 2018, kwenye Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma, nilizindua Kampeni ya Kuhamasisha Umma wa Watanzania kupima VVU na kuanza dawa za kufubaza VVU mara wanapogundulika na maambukizi, mpango uliojulikana kama *Test and Treat*. Kampeni hii inakwenda sambamba na kauli mbiu ya ujumla isemayo, 'Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi'. *(Makofî)*

Mheshimiwa Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kampeni hiyo ya siku tano kwa wakazi wa Jiji la Dodoma imewezesha watu 4,725 kupima afya zao na kujitambua ambapo kati yao wanaume walikuwa 3,061 na wanawake walikuwa 1,664. Hii maana yake wanaume wameanza kuhamasika kupima VVU. Aidha, kupitia kauli mbiu ya, 'Mwanaume Jali Afya Yako, Pima VVU', mimi niliridhia kuwa kinara wa kuhamasisha wanaume kupima na kuanza dawa mapema kwa wale wanaogundulika kuwa na maambukizi ya VVU. *(Makofî)*

Mheshimiwa Spika, hali ya kujinginga na maambukizo ya VVU nchini bado siyo ya kuridhisha sana. Mathalan, hadi kufikia Machi, 2018, jumla ya watu wanaoishi na VVU ilikuwa ni 1,022,745. Kati yao, watu 1,007,026 walikuwa wanatumia dawa za kufubaza VVU.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inatekeleza malengo ya 90, 90, 90 ifikapo mwaka 2020 katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI. Tisini tatu zina lengo la kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU wawe wamejua hali zao za maambukizi; asilimia 90 ya wanaopima VVU na kugundulika kuwa wana maambukizi wapatiwe dawa za kufubaza VVU na asilimia 90 ya watu wanaotumia dawa wawe wameshafubaza VVU. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitumie pia nafasi hii kuendelea kuhamasisha wananchi wapime VVU. Nitumie nafasi hii pia kukupongeza wewe mwenyewe kwa kushiriki kikamilifu katika kampeni ya upimaji na kuongoza Waheshimiwa Wabunge katika upimaji wa hiari siku tarehe ya 21 Juni, 2018. Jambo hili ni muhimu kwetu sisi viongozi. Aidha, kufuatia zoezi hili, wale watakaogundulika wana maambukizo ya VVU waanze mara moja kutumia dawa za kufubaza. Waheshimiwa Wabunge wenzangu nasi pia na katika majukwaa yetu ya kisiasa, moja kati ya agenda iwe ni kuunga mkono kuhamasisha Watanzania kwa kuendelea kuitamka kauli mbiu ya "Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi" ili Watanzania wote wajitokeze kupima VVU mahali popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hitimisho, katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019 kwa mafanikio, napenda kusisitiza mambo yafuatayo nikiwa nahitisha hotuba yangu.

(i) Uwajibikaji na nidhamu kwa watumishi wa umma katika kuhudumia wananchi hususan wale wa vijiji;

(ii) Taasisi zote ziimarishe mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili ikamilike kwa wakati na kuwanufaisha Watanzania;

(iii) Kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Mpango wa Kilimo wa Awamu ya Pili (*ASDP II*) ili uweze kuleta mapinduzi ya kilimo na tija kwa wakulima sambamba na kuchangia ukuaji wa sekta ya viwanda;

(iv) Matumizi ya mifumo ya kielekroniki katika kutoa huduma mbalimba kwa lengo la kuondoa urasimu usiokuwa wa lazima katika utoaji huduma kwa wananchi;

(v) Kuendelea kutumia *EFD* katika ukusanyaji wa mapato;

(vi) Kuendeleza ushirikiano baina ya Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo; na

(vii) Viongozi, watendaji na wananchi wote kuifanyia kazi kauli mbiu ya mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ya ,‘Furaha Yangu, Pima, Jitambue, Ishi’.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe yangu kwa kuwatachia safari njema Waheshimiwa Wabunge wote mnaporejea Majimboni kwenu kuwaeleza wananchi mambo yaliyojiri hapa Bungeni. Waelezeni wananchi matarajio yetu kwa na kuwasih i waendelee kutuunga mkono kwenye tijihada zetu zinazopelekea mazingira wezeshi ya kujikwamua kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru Watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu kwa weledi, maadili na ufanisi mkubwa. Aidha, nawashukuru wanahabari kwa uchambuzi wao wa hoja zilizokuwa zikiendelea Bungeni na kufikisha habari hizo kwa wananchi. Nivishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili pamoja na wageni wetu bila kuwasahau madereva waliotuhudumia wakati wote, wametuleta Bungeni na bado watatufikisha Majimboni kwetu na naamini tutaendelea kuwa salama. Tunawashukuru sana madereva wote kwa kazi mzuri mnayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunataraja kwamba tarehe 22 Agosti, 2018 kutegemeana na mwandamo wa mwezi, kutakuwa na Sikukuu ya Eid Al-Haj. Natumia fursa hii

kuwatakia Waislamu na Watanzania wote nchini maadhimisho mema ya siku hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 4 Septemba, 2018, siku ya Jumanne saa 3.00 asubuhi litakapokutana tena kwenye ukumbi huu ulioko Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU, BUNGE NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na sijawahi kuona hoja imeungwa mkono kama hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu umeungwa mkono kweli kweli. Waheshimiwa Wabunge wamechoka kabisa kukaa hapa Dodoma. (*Makofî/Kicheko*)

Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyoweka *summary* ya shughuli zote ambazo tumezifanya kwa miezi hii mitatu hapa Dodoma. Tunakushukuru sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, sijui hata kama kuna haja ya kuhoji kuhusu hoja hii maana wote mmeunga mkono kwa kusimama lakini kwa sababu ni utaratibu basi naomba niwahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Nadhani walioafiki wameshinda. (*Kicheko/Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati *Brass Band* inajiandaa, napenda niseme maneno machache tu. Naomba kila Mbunge anapoondoka tupite pale *pigeonhole*

na kwa kweli tuchukue *documents* zetu nyingi kadri tunavyoweza.

Mtakumbuka wakati wa Bunge hili tumefanya semina nyingi sana kwa kila Kamati, tumeppata elimu kubwa sana. Tutaendelea kufanya hivyo kadri hali itakavyoruhusu uko mbele. Tunawashukuru wote ambao walikuja hapa na kutufanyia uwezeshaji.

Katika Bunge hili Waheshimiwa Wabunge mmechangia kila hoja na mada zilizoletwa hapa. Kwa kweli Wizara zinaondoka zimesheheni ushauri wa Wabunge wa kila aina. Ni wajibu wao kutazama ule ambao unafaa kufanyiwa kazi, basi wakaufanyie kazi. Sisi kama Bunge wajibu wetu wa kuishauri Serikali kwa kweli tumeufanya na tumewawezesha mafungu, sasa tushirikiane nao tuone namna gani tutapiga hatua zaidi katika nchi yetu. Yote ambayo tumeyashauri yako kwenye *Hansard*, kwa yule ambaye anahitaji *reference* yoyote, tuko vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, hizi *Hansard* ni moja ya kumbukumbu muhimu za Taifa. Ukitaka kujua nchi hii imetoka wapi, imekuwa wapi na inaenda wapi, moja ya vitu ambavyo unaweza uka-refer ni *Hansard* za Bunge. Kwa mfano, ukichukua *Hansard* zile za miaka ile ya 1960, 1961, 1962 wakati nchi inapata uhuru 1965 mpaka 1967 hivi, utaona aina ya Kiswahili kilichokuwa kinatumika wakati huo; utaona aina ya hoja za enzi hizo, utapata picha nchi ilikuwa inafananaje kwa kuangalia tu wale Wawakilishi wa wakati ule walikuwa wanazungumza nini na Serikali ya wakati ilikuwa ikielekeea wapi na kadhalika.

Kwa hiyo, nasi wa Bunge la Kumi na Moja wenzetu watakaokuja baada yetu huko mbele sana, wakija kuangalia mambo yetu ya Bunge kama hili, mtu akipitia *Hansard* mwanzo mpaka mwisho kwa mambo yaliyoongeleta hapa, anapata picha nchi ya nchi hii hivi sasa iko wapi. Kwa hiyo, *Hansard* zinatusaidia sana, tunashukuru. Katibu uendelee kuiimarisha Idara hii ya *Hansard* kwa sababu ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunamaliza Bunge hili la Kumi na Moja kifupi kama Bunge la Korosho, maana *issue* ya korosho iliwaka moto kweli kweli humu ndani, lakin tumefika pazuri, tumeishauri Serikali, Wizara ya Kilimo wametuhahidi kabisa mambo yatakuwa mswanu. Kwa hiyo, tunatarajia wote ambao tumewaa mini kuwaachia jambo hili la korosho watajipanga vizuri na mazao mengine ili yaweze kwenda vizuri kama wote ambavyo tunarajia. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu ametukumbusha hapa habari ya kupima Virusi vya Ukimwi (VVU) na tunampongeza ye ye mwenyewe aliongoza jambo hili kwa kupima wa kwanza, nami nikamuunga mkono nikapimwa na wenzangu baadhi mkafanya hivyo hivyo lakini baadhi walilingia mitini. Sasa ombi letu ni kwamba tunapoenda Majimboni hii iwe ni moja ya ajenda zetu ambazo tutazifliksha kwa wananchi wetu. Janga hili bado ni kubwa, ni lazima tushiriki katika kupeleka ujumbe huo ili watu wetu wajifahamu na wakishajifahamu maana yake wataji-*position* katika namna ya kupata huduma ile ilio bora. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, naishukuru sana Serikali, tumekuwa pamoja toka Aprili, tunashukuru sana. Tunajua *participation* ya Mheshimiwa Rais ilikuwa kubwa, Waheshimiwa Mawaziri wote mkiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunasema ahsanteni sana. Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Maafisa wote wa Serikali mmeピta kwenye kikaango kigumu lakini tumefika mwisho salama. Yote ni kwa nia njema kuona kwamba nchi inakwenda vizuri. (*Makof*)

Nawashukuruni sana Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo mlikuwa mkifuatilia kwa karibu, mlikuwa mkichangia, wengine kwa uchungu, watu mpaka wametoa machozi humu ndani. Hiyo yote ni kuwasilisha hisia, kwa kweli mtu hawezu kurudi kwa wananchi akiwa hana cha kueleza. Kwa hiyo, tumepata picha ya nini ambacho kinatakiwa, tunaondoka hapa tukiwa bora zaidi kuliko tulivyokuja.

Nazishukuru sana Kamati zote za Bunge kwa kazi nzuri ambazo zimefanya, pamoja na viongozi wa Kamati hizo, Wenyevit na Makamu. Makamishina wote wa Tume ya Bunge, nasema ahsanteni sana kwa kazi ambayo tumekuwa tukifanya. Kamati ya Uongozi tuliwaita kila wakati, tulikaa, tukaamua na tukashauri, nawashukuruni sana. Bila Kamati ya Uongozi tusingeweza kufika hapa tulipofika.

Katibu wa Bunge, tunakushukuru sana pamoja na timu yako yote. Waheshimiwa Wabunge, katika wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwa bidii sana ni pamoja na wafanyakazi wa Bunge, kabisa kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ni ofisi chache ambazo watumishi wake wanafanya kazi wakati mwingine mpaka saa 8.00, saa 7.00 au saa 4.00 usiku, lakini kwa Ofisi za Bunge ni jambo la kawaida. Tunapokuwepo hapa hawana sikuu wala Jumapili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Katibu kwa kweli utupelekee salamu kwa watumishi wote wa Bunge. Umesikia Katibu wanasema na posho yao ya safari hii hebu iangalie vizuri. Tunawashukuru sana, sana, sana. (*Makofi*)

Waandishi wa Habari wote mlioshiriki pamoja nasi tunawashukuruni sana. Mmepeleka habari kwa wananchi tunawashukuruni sana. (*Makofi*)

Nashukuru sana zile Kamati za Spika mbili ambazo mliitoa ripoti zenu safari hii; Kamati ya Uvuvi wa Bahari Kuu na Kamati ya Masuala ya Gesi ya Mheshimiwa Anastazia Wambura na ya Mheshimiwa Mheshimiwa Kitandula. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mliifanya na mawasilisho mazuri sana. (*Makofi*)

Tunawashukuru sana *TWPG* kwa siku ile maalum. Wale wenzetu wanasema *you made our day*, yaani mlionyesha maajabu kabisa. Tukaona kumbe tuna vipaji vingi miongoni mwetu, tukawaibua akina Mweshimiwa Ali King. Mheshimiwa Sugu na Mheshimiwa Mbunge wa Mikumi bado

hawajaonekana kwenye *stage*, kwa hiyo, hizi *talent* tumeziweka za akiba, kwenye hii inayoandaliwa Dar es Salaam naamini kabisa itakuwa moto zaidi. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Kwaya ilikuwa nzuri sana ikongozwa na Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Vicky Kamata. Mheshimiwa Ungando, singeli ile ilikuwa hatari kabisa. Mheshimiwa Massay na wenzake kwenye sarakasi ilikuwa hatari. Kwa maoni yangu waliotia fora kuliko wote ni wale wa miondoko ya *miss* na hasa Mheshimiwa Asha Abdallah Juma (Mshua) na Prof. Anna Tibaijuka ilikuwa hatari. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Kwa kweli tunawashukuru wote na kwa kuwa ilikuwa ni uzinduzi, basi jambo hili litaendelea ili tufikie ndoto yetu ya kwamba kila Jimbo la Tanzania angalau tupate choo kimoja cha mfano ambacho ni choo rafiki kwa matumizi ya watoto wa kike na wale wenye mahitaji maalum. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Pia tulipata ugeni wa ndugu yetu Mbunda, wale maharusi wa mfano kabisa na mkasema hapa kwamba tuwachangie Sh.20,000 kwa kila Mbunge na mchango wetu ambaao tuliuchangisha na ameshakabidhiwa, nitangaze kwamba ni Sh.7,840,000 na tumekwishawapatia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Liwale ambaye ndiye Mbunge wao, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka. (*Makofi/Vigelegele*)

Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wasaidizi wangu hapa Meza Kuu wakiongozwa na Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, ahsante sana, sana; Mheshimiwa Chenge ahsante sana, nakushukuru sana kwa kazi kubwa ambayo umeifanya; Mheshimiwa Najma tunakushukuru sana, ahsante sana; Mheshimiwa Zungu ahsante sana, sana. Kwa kweli kwa pamoja tumeweza kufikisha gurudumu hili hapa mwisho. Nawashukuruni mno na tuendelee kufanya kazi kwa pamoja kwa nguvu zaidi kadri Mungu atakavyotujalia. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, Tume ya Huduma za Bunge tutakutana leo kuanzia saa 6.00 kwenye ukumbi wa Spika pale.

Mwisho, niwatakie kila la kheri, twende taratibu taratibu Waheshimiwa Wabunge. Tunapoondoka hapa, madereva wetu tuwaambie waende kwa *speed ambayo ni* ya kirafiki, tutafika tu safari yetu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

WIMBO WA TAIFA

SPIKA: Naomba tusimame sasa ili tuwakaribishe *Brass Band* ya JKT Makutupora waweze kutuongoza katika Wimbo wa Taifa. Tukumbushane wote tulikubaliana wote tutakuwa *attention* na siyo vinginevyo. Karibu sana JKT.

(*Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi tarehe 4 Septemba, 2018.

(*Saa 5.44 Asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 4 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi*)